

KISWAHILI



**SANIFU KWA SHULE
ZA SEKONDARI**

**KITABU CHA MWANAFUNZI
KIDATO CHA NNE MKONDO WA LUGHA**



YALIYOMO

UTANGULIZI	iv
SURA YA KWANZA: HISTORIA YA KISWAHILI	1
SURA YA PILI: FASIHI	11
DHIMA YA FASIHI	12
SURA YA TATU: NGELI ZA MAJINA	42
SURA YA NNE: USEMI HALISI NA USEMI WA TAARIFA	70
SURA YA TANO: UTUNGAJI	73
SURA YA SITA: AINA ZA MANENO	78

UTANGULIZI

Kunapita wakati wa kotosha Wanyarwanda walikuwa na hamu ya kujifunza lugha ya Kiswahili lakini shida ilikuwa ni ukosefu wa vitabu vinavyoandikwa katika lugha hiyo kwa ufasaha. Ikumbukwe kuwa kazi ya kuandika vitabu si jambo rahisi kwa kila mtumiaji wa lugha.

Wakati huu Kiswahili kina umuhimu sana katika jamii ya Afrika na hata katika ulimwenguni kote. Hii ni lugha rahisi kuitamka kutokana na mtindo wake kama lugha nyingine za kibantu.

Kitabu hiki ambacho ni “*Kitabu cha mwanafunzi kidato cha nne*” kinaundwa na sehemu kuu 6 ambazo ni: **historia ya Kiswahili, fasihi, ngeli za majina, usemi halisi na usemi wa taarifa, utungaji na aina za maneno**. Kitabu hiki kitasaidia katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule zinazofundisha lugha kikiwemo Kiswahili. Kitatilia mkazo matumizi ya Kiswahili katika maisha ya kila siku kwa wale wanaohitaji kuelewa na kutumia Kiswahili ipasavyo.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa ajili ya kuziba pengo la ufundishaji wa Kiswahili na kumaliza mahitaji ya walimu na wanafunzi. Kitabu hiki kimejaribu kuishughulikia miundo tofauti ya lugha ya Kiswahili kwa urefu na kuondoa utata unaojitokeza katika kusoma na kufundisha Kiswahili.

Kitabu hiki kimeandikwa na **NDAYAMBAJE Ladislav na NIYIRORA Emmanuel** ambao ni walimu kutoka Chuo Kikuu cha Elimu cha Kigali. Ndani mwake tulitoa maelezo ya kila mada inayounda kitabu hiki pamoja na mazoezi yatakayowafanya wanafunzi kukua kiakili na kijamii

Katika kitabu hiki tunadhamiria kuwaeleza wanafunzi namna ya kutumia historia ya Kiswahili, sarufi ya Kiswahili, fasihi pamoja na maandishi mbalimbali kwa kuendeleza maisha yao ya kesho.

Pamoja na haya, maswali maridhawa ya kufanyia mazoezi yametolewa ili kumshirikisha mwanafunzi moja kwa moja na yale anayojifunza.

NDAYAMBAJE Ladislav

NIYIRORA Emmanuel

SURA YA KWANZA: HISTORIA YA KISWAHILI

1.1. NADHARIA TETE KUHUSU ASILI NENO KISWAHILI

Nadharia tete au chukulizi hutumia kuelezea mawazo fulani aliyonayo mtafiti kabla ya kufanya utafiti. Mawazo haya huweza yakathibitishwa au yasithibitiswe. Pia haihypothesia (Wamitila 2003).

Asili ya neno “**Kiswahili**” ni Kiarabu “**Swahel**” lenye maana ya ukanda wa ardhi iliyolimwa yenye miji au vijiji vilivyoko kando kando ya bahari au mto mkubwa. Kuna nadharia mbili kuhusu neno Kiswahili :

1. **Nadharia ya kwanza** ni ile isemayo kuwa Kiswahili ni neno lenye viambishi **Ki-swahel** kumaanisha watu wa pwani au mwambao yaani sehemu za kando ya mto au bahari. Kwa hiyo Kiswahili ni lugha ya watu wa pwani.
2. **Nadharia ya pili** ni ile isemayo kwamba Kiswahili ni neno lenye viambishi **Kisiwa-hila** kumaanisha watu ambao ni wenye sifa ya ujanja, ukorofi n.k. Yaani watu wanaotumia Kiswahili kwa kunyang'anya mali za watu (Wahuni). Kwa hiyo, kutokana na nadharia hizi mbili na uchunguzi wa historia ya lugha ya Kiswahili, tunaona kuwa Kiswahili humaanisha watu wa pwani. Watu ambao hutumia lugha yenyewe ya Kiswahili.

Baadhi ya watu hudai kwamba tunazo nadharia kadhaa kuhusu historia ya lugha ya Kiswahili lakini tukichunguza kile wanachoita nadharia, tunagundua kwamba hizo bado ni nadharia tete hazijakuwa nadharia hasa. Kuna nadharia tete nne ambazo ni muhimu.

Nadharia tete ya kwanza ni ile isemayo kwamba Kiswahili kimetokana na lugha ya Kiarabu, ya pili ni ile isemayo kuwa Kiswahili kimetokana na mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu na lugha za Kibantu zilizokuwa katika Upwa wa Afrika ya Mashariki, ya tatu inasema kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu iliyoathiriwa na lugha ya Kiarabu, ya mwisho ni ile isemayo kwamba lugha ya Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha kadhaa za Kibantu zilizokua katika Upwa wa Afrika ya Mashariki na ikaathiriwa sana na Kiarabu kimsamiati katika kukua kwake.

1.1.1. KISWAHILI KUTOKANA NA KIARABU

Hapa kuna madai (nadharia) mawili kuwa:

1. Kiswahili ni pijini ya Kiarabu.
2. Kiswahili hutoka sehemu za pwani, na watu wa pwani ni Waislamu, uislamu uliletwa na Waarabu kwa hiyo Kiswahili ni lugha ya Waarabu.

Kwa upande mwingine madai haya ni butu kwa sababu Kiswahili si pijini wala ni lugha ya Kiarabu bali yoyote inaweza kutumia maneno ya mkopo kutoka lugha nyingine. Kwa hiyo lugha mbili au zaidi huweza kuathiriana. Huu ndio ukweli kwa lugha ya Kiswahili.

1.1.2. KISWAHILI KUWA LUGHA CHOTARA

Dai hili linasema kuwa Kiswahili ni lugha chotara, yaani ni lugha inayochanganya **Kiarabu** na **lugha ya watu wa pwani**, kwa hiyo wakasema kuwa Kiswahili ni pijini. Katika pijini mtu anatumia maneno kivyake tofauti na mwingine, kilichomuhimu ni kuwasilisha ujumbe. Wakati watu hawa wanaotumia pijini wanafaulu kuunda muundo wa maneno, mofolojia, fonolojia, sentakisia pijini hubadilika Krioli.

Hapa tunaweza kusema kuwa huu ni ukweli kwa Kiswahili, lakini swali likazuka. Krioli ni lugha ambayo ina muundo, mofolojia, sentakisia ambavyo ni pekee, visivyohusiana na lugha nyingine. Lakini Kiswahili si Pijini kwa sababu ni lugha ambayo huhusiana na lugha za Kibantu.

Watetezi wa nadharia tete hii kama akina Hamo Sassoon wanakiri kabisa kwamba msamiati wa lugha ya Kiswahili ni asilimia 80 Kibantu. Tukizingatia yote haya tunaona kwamba hatuna sababu ya kutushawishi kukubaliana na nadharia tete hii.

1.1.3. KISWAHILI KUTOKANA NA KIBANTU

Wanaisimu wanasema kuwa kuna nadharia tete nne kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili. Mbili miongoni mwa hizo zimeishazungumziwa. bNyingine za mwisho zinahusiana yaani ile isemayo kwamba Kiswahili ni lugha ya kibantu na ile isemayo kuwa Kiswahili ni lugha iliyoibuka kutokana na mchanganyiko wa lugha kadhaa za kibantu zilizokuwa Pwani. Nadharia hizi zote zinahusiana kwa sababu ukichunguza lugha za Kibantu,

hutumia taratibu ya kuunda maneno sawa na lugha kadhaa za kibantu zilizokuwa pwani. Ni kusema kwamba maumbo ya maneno katika lugha hizi mbili ni sawa. Lugha hizi zote zina viambishi vya mwisho, kati na vya awali. Kutokana na haya Kiswahili hutokana na lugha za Kibantu.

1.2. HISTORIA YENYEWWE

Lugha yoyote, hasa lugha iliyo hai na inayokuwa inatokana na mazingira maalum ya watu na utamaduni wao. Kiswahili ni lugha ya Afrika ya Mashariki iliyoenea na kujulikana na wengi zaidi katika Afrika ya Mashariki kuliko lugha nyingine yoyote ya Afrika. Kuna wakati, na pengine mpaka leo ambapo lugha hii ilikuwa ikiambiwa eti ni ya kigeni, yaani asili yake si Afrika. Hivi leo ni wachache ambao wana mawazo hayo, nao hawayatamki kwa kuchelea kuthibitisha kuwa ni wajinga wa historia na mambo yalivyo. Maana jambo hilo kuwa Kiswahili ni lugha ya kienyeji, linathibitishwa kabisa basi na kubakisha chembe ya shaka.

1.2.1. KISWAHILI KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI

1.2.1.1. AFRIKA YA MASHARIKI KABLA YA UKOLONI

Maandishi mengi ya wanakimapokeo na kimaghalibi yanatuambia kwamba Kiswahili si Kibantu bali ni lugha ya Kiarabu pia inatokana na wageni. Na wakaendelea kusema kuwa Kiswahili kilienezwa na wageni waliokuja kufanya biashara na kutangaza dini zao. Lakini kauli hii si tabithi kwa sababu kabla ya kufika kwa wageni na ukoloni wa Kiarabu na Kizungu, Kiswahili kilikuwepo. Wenyeji wa pwani na wenyeji wa bara walikuwa na muasala wa ya kufika kwa wageni kulikuwa na safari za kibiashara, za mawasiliano baina ya pwani na bara zilizokuwa zikifanywa na Waafrika wenyewe.

1.2.1.2. AFRIKA YA MASHARIKI WAKATI WA UKOLONI

Wageni waliingia katika Afrika ya Mashariki na kuathiri lugha hiyo ya Kiswahili kwa njia moja au niyingine. Koloni la Ujerumani lilianzishwa Tanganyika lakini likapingwa sana na wenyeji mfano ni vita vya Maji Maji na vita vya BUSHIRI.

Wajerumani walitawala na kuanzisha shule ya kwanza Tanga mnamo 1895 ya kuandaa watumishi wa kiafrika. Katika mwaka 1903 Kiswahili kilitiliwa mkazo

serikalini, makanisani na shuleni. Wajerumani walikiona Kiswahili muhimu sana kwa kuendeleza ukoloni wao, kwa hiyo Wajerumani wao wenyewe walijifunza Kiswahili na kukitumia mfano Magavana kama RECHEMBERG(1900-1912) na H.SCHENCE. Wakoloni hawa walikitumia hasa katika kuandika magazeti kama ***Msimulizi*** (1888) na ***Habari za Mwezi*** (1894) pia walikitumia kwa kutafsiri vitabu. Mfano ni LUDWIG KRUPF alietafsiri ***Injili ya Luka na Yohani*** katika Kiswahili na aliandika mhusara wa sarufi na msamiati ili kazi hiyo ianze kuwasaidia Wamishenari. Dkt KRUPF aliendelea na kazi hiyo akaandika ***Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza***.

Huyu LUDWIG ndie alieanzisha **CHURCH MISSION SOCIETY** huko Mombasa na alijifunza Kiswahili na kuandika kwa hati ya Kilatini. Wakoloni hawa walieanzisha shule nyingi huko Tanganyika. Mnamo 1925 Kiswahili kiliteuliwa kutumiwa katika elimu, toka wakati huo Kiswahili kikatumiwa huko Tanganyika mashuleni. Mnamo 1928 kukawa mkutano kuhusu utumiaji wa Kiswahili wa wawakilishi wa Unguja, Kenya, Uganda na Tanganyika. Walikuwa huko Mombasa na lahaja ya Kiunguja ikapitishwa kuwa itumiwe Afrika ya Mashariki. Waziri wa makoloni na Uingereza alitoa amri ya kuanzisha Baraza la Kiswahili kwa ajili ya nchi zote nne yaani Uganda, Kenya, Unguja na Tanganyika. Tarehe 1 Januari 1930 ikaundwa Kamati iliyojulikana kwa jina la **“Inter-territorial language (Swahili) Committee”** na shabaha yake kuu ilikuwa kusanifisha lugha ya Kiswahili na kuondoa lahaja zilizokuwepo. Chini ya halimashauri hiyo: Kamusi mbili zilitengenezwa **“Standard”Swahili-English** na **English-Swahili**. Katika jitihada hiyo ya kusanifisha, ndipo watu kama Canon BROOMFIELD wakajitokeza kuandika Kamusi na sarufi ya Kiswahili.

1.2.1.3. AFRIKA YA MASHARIKI WAKATI WA HARAKATI ZA UHURU

Wakati wote wa Ukoloni, Kiswahili kilikuwa kiungo kati ya tawala za Wenyeji, za Wilaya na serikali ya Kikoloni. Wakati wa harakati, wanasiasa walijaribu kutumia Kiswahili kama kiungo kati yao na wananchi.

TANGANYIKA

Kiswahili japo kimeonekana madarasani kwa watawala na raia kuwa ni lugha duni, lakini wanasiasa walikitumia sana. Mnamo 1922 Chama cha Wafanyakazi wa Serikali (Tanganyika Territory Civil Servants Associations) kilianzishwa huko Tanga.

Tanganyika African Association (TAA) kilianzishwa Dar-es-Salaam na kusambaa nchi nzima. Chama kilikuwa na Katiba yake katika Kiswahili. Kiswahili kikatiliwa mkazo sana. Mnamo 1954, TAA kikabadilishwa na kuwa TANU (Tanganyika African National Union). Na kiongozi akawa Mwalimu Julius Kambarage NYERERE. Mara nyingi mikutano yake ya hadhara alikitumia Kiswahili bila ya mkalimani. Mnamo 1955, Kiswahili kilianza kutumiwa Bungeni. Na 1961, TANU ikafanya Kiswahili kuwa lugha ya kitaifa. TANU ilijaribu sana kukikuzi na kukitumia Kiswahili na watu wakaanza kuitumia sana lugha hii. Wakati huu wote Kiswahili kilikuwa ni chombo muhimu cha kuleta ukombozi wa kisiasa nchini.

KENYA

Nchini Kenya, chimbuko la Kiswahili ni Pwani. Wakati wa Ukoloni japo walikuwepo magavana ambao waliunga mkono kwa dhati raia kukitumia Kiswahili. Lakini Kiswahili kilipigwa vita sana. Kwa mfano mnamo 1900 SIR CHARLES ELIST aliyekuwa Gavana alihimiza lugha za makabila mengine na hakutaka Kiswahili kutumiwe. Lengo lake kubwa ni kuifanya Kenya iwe chini ya Wazungu na hakutaka kiungo chochote cha lugha ya Kiafrika. Hali hii iliendelea sana mnamo 1935 Kiingereza kikawa lugha ya mtihani katika Shule ya msingi na mwaka huo kukakuwepo na Tume ya Kifalume ya Afrika ya Mashariki ya kutoa ushauri wa matumizi ya lugha mashuleni hata hivyo wanasiasa walijalibu sana kukitilia mkazo Kiswahili toka awali, na pole pole kikaanza kuwaunganisha wananchi katika harakati za Ukombozi.

1.2.1.4. KISWAHILI WAKATI WA UHURU

Kiswahili wakati wa uhuru kimechanua na kukua sana. Baada ya uhuru, mataifa yote matatu ya Afrika ya Mashariki yametilia mkazo lugha hii ya Kiswahili.

Tanzania, Kiswahili ni lugha ya taifa. Inafundishwa toka shule za msingi hadi chuo kikuu kama lugha. Lipo Baraza la Kiswahili la taifa la kukuza lugha hii na ipo taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili ambayo hutoa majarida na kuendesha utafiti. Kiswahili ndiyo lugha ya kazi na biashara na ndiyo inayotumiwa Bungeni. Katika Kenya toka 1993, Kiswahili hutumiwa Bungeni. Hayati Mzee Jomo KENYATTA, wakati wote alikuwa anatumia Kiswahili na kukihimiza. Kiswahili ni lugha ya taifa Kenya. Pia hufundishwa toka Shule za msingi hadi Vyuho Vikuu. Nchini Uganda, Kiswahili hufundishwa sekondari na katika Vyuho vikuu.



1.2.1.5. KISWAHILI BAADA YA UHURU

Baada ya uhuru lugha ya Kiswahili ilifanywa kuwa ndiyo lugha ya taifa katika mataifa ya Tanganyika na Kenya. Watu wote katika nchi hizi walilazimishwa kutumia Kiswahili sehemu zote na kikafundishwa kutoka darasa la kwanza hadi la nane. Kutokana na umuhimu wa lugha hiyo, mnamo mwaka 1967, serikali ya Tanganyika (Tanzania ya wakati huu) ikatamka rasmi kuwa lugha ya Kiswahili itumike pia kama lugha rasmi ikienda sambamba na lugha ya Kiingereza. Ndipo palianzishwa BAKITA (Baraza ya Kiswahili la Taifa) ambalo lilipewa kazi ya kuratibu shughuli zote za ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kote nchini.

Mnamo 1969, Rais wa Kenya Mzee Jomo Kenyatta alitoa kauli kwamba lugha ya Kiswahili ilifaa kutumika kama lugha rasmi katika nchi ya Kenya. Alitoa amri kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya mawasiliano katika Bunge. Kiswahili kilifundishwa pia katika vyo vikiu.

1.2.2. KISWAHILI KATIKA DRC, BURUNDI, NCHI NYINGINE ZA AFRIKA NA ULIMWENGUNI

1.2.2.1. Kiswahili katika DRC

Tipu-Tipu (mfanya biashara), kabla ya 1860, alifanya safari za biashara sehemu ya mashariki ya D.R.C. Safari yake ya awali alifika Urua ng'ambo ya ziwa Tanganyika. Misafara hii ikazidi kuwa mingi na kusambaza Kiswahili Mashariki ya Kongo. Wafanyabiashara walitumia Kiswahili katika kazi yao. Wenyeji walitumia lugha ya Kiswahili wakapachikwa jina la Waungwana wa lugha ya Kiswahili. Uungwana wao ulikuwa katika kusema Kiswahili. Kiswahili chao kiliathiriwa sana na Kifaransa na Kimanyema na kwa kuwa waliitwa waungwana na Kiswahili chao kikaitwa Kiingwana. Wabeligiji wakatumia Kiswahili kwa kuwatawala Waungwana. Hivi Kiswahili kikaenea nchini miongoni mwa askari na katika mashimo ya Shaba (Katanga). Misheni za Kibeligiji nazo zilitumia Kiswahili katika shughuli zao na vitabu na magazeti.

Katika DRC, kuna lugha Kama 200 za Kibantu na kati ya hizo lugha rasmi zinazotumiwa katika nchi ni Lingala, Luba, Kikongo na Kiswahili. Lugha ya Kifaransa, ambayo si lugha ya Kibantu, nayo hutumiwa kama lugha rasmi nchini D.R.C. Na hata katika hicho

Kiswahili cha huko Kongo kiitwacho Kingwana ipo tofauti ya Kiswahili cha Katanga na kile kisemwacho Kisangani. Hata hivyo, chini ya uongozi wa Hayati Rais MOBUTU Seseko kulikuwa jitihada ya kueneza na kukikuza Kiswahili pia na kutumia Kiswahili sanifu.

1.2.2.2. Kiswahili katika BURUNDI

Wasafiri waliopita D.R.C., walipitia Burundi na kuiathiri sana katika kutumia Kiswahili toka enzi za majilio ya wageni na Wakoloni. Baada ya uhuru, Burundi wanafundisha Kiswahili katika chuo kikuu na kutumia Kiswahili katika Redio Burundi, IBYIZIGIRO, ISANGANIRO, TELEVISHENI na magazeti mbalimbali. Kuna idadi kubwa ya Wananchi wa Burundi ambao hutumia Kiswahili kwa sababu ya kuathiriwa na majirani wa Tanzania na D.R.C.

1.2.2.3. Kiswahili katika nchi nyingine za Afrika

Katika Afrika, si nchi hizo tu zinazothamani Kiswahili kama lugha mojawapo ya Afrika. Visiwa vya Komoro hutumia Kiswahili na baadhi ya vipindi vya redio hutangaza habari katika Kiswahili. Sudan, Kiswahili kinafundishwa katika Chuo kikuu kimoja. Kiswahili kinachofundishwa huko ni Kiswahili sanifu.

Msumbiji wapo wazungumzaji wa Kiswahili. Katika Chuo cha mambo ya Afrika ya kusini hutangaza katika Kiswahili baadhi ya vipindi vyao vya redio. Ghana, Guinea, Nigeria na Libya wameamua kufundisha Kiswahili sanifu katika vyuo vikuu vyao. Mpakani mwa Zambia na Tanzania huzungumza Kiswahili, pia mpakani mwa Zambia na Kongo.

1.2.2.4. Kiswahili ulimwenguni

Kiswahili kimeenea sehemu mbalimbali nje ya Afrika. Uingereza katika Chuo cha mambo ya Afrika kuna maktaba kubwa ya Kiswahili. Lugha hiyo hufanyiwa utafiti. Huko Marekani kuna vyuo mbalimbali ambavyo hufundisha Kiswahili. Na baadhi ya vyuo duniani vinavyofundisha Kiswahili ni:

- ✓ Universit t Hamburg
- ✓ Seminar f r Afrikanische Sprachane Und Kulfuren.
- ✓ Philips-Universit t Marburg

- ✓ Université Paris III Institut National des Langues et civilisations orientales(INALCO)
- ✓ Institut de linguistique
- ✓ University of London
- ✓ School of Oriental and African Studies
- ✓ University of YORK Department of Language.

Utaona hata hivi ambavyo tumeviandika hapa si vichache katika dunia. Kuna vyuo vingine zaidi ya sitini na nne ambavyo hufundisha Kiswahili duniani kote.

Kuna idhaa za Kiswahili katika redio duniani takribani ishirini na tisa zinazotangaza kwa lugha ya Kiswahili:

- ✓ Idhaa ya Kiswahili ya BBC ya sauti ya Amerika
- ✓ Idhaa ya Kiswahili ya sauti ya Kijerumani
- ✓ Idhaa ya Kiswahili ya redio Japan kama taifa Jeram-Fehran.

1.3. LUGHA ZA KIGENI KUATHIRI KISWAHILI

Athari ya Wareno inaonekana katika lugha ya Kiswahili ambamo mna maneno ya Kireno yaliyomezwa na kuwa ya Kiswahili.

Kireno	Kiswahili
Mesa	Meza
Lenso	Leso
Caraco	Korosho
Seti	Seti
Espada	Shupaza
Carta	Karata
Vinho	Mvinyo

Mifano ya maneno ya Kiarabu yaliyomezwa katika Kiswahili.

Neno lenye asili ya Kiarabu	Kiswahili asilia
Daimat	Milele
Hidashara	Kumi na moja
Yamini	Kiapo
Ila	Isipokuwa
Sabiki	Tangulia
Ratibu	Panga
Tisa	Kenda
Nadra	Tukizi
Wahedi	Moja
Swalah	Sala
Khabar	Habari

Siyo Waarabu na Wareno peke yao walioathiri Waswahili hata Wajemi, Wahindi, Waturuki, n.k. walifanya hivyo. Ndiyo sababu tulipata maneno kutoka kwa lugha za watu hawa yaliyolingia katika Kiswahili.

Kiajemi	Kiswahili
Baftah	Bafta
Balunk	Balungi
Bandar	Bandari
Darbyn	Darubini
Diricha	Dirisha
Kwurdun	Gurudumu
Karan	Karani
Kod	Kodi
Pilao	Pilau
Randah	Randa
Rushn	Roshani

Kihindi	Kiswahili
Bhangri	Bangili
Bhajiya	Bajia
Biyama	Bima
Dhobi	Dobi
Ghadi	Gari
Hundir	Hundi
Lakh	Laki
Paisa	Pesa
Rang	Rangi
Tumbaku	Tumbaku

Kituruki	Kiswahili
Balyus	Balozi
Baashawishi	Bishaushi
Bughsha	Bahasha
Caixa	Kasha
Efendy	Afendi
Kohkoni	Korokoroni

MAZOEZI

1. Eleza asili ya Kiswahili.
2. Eleza ubantu wa Kiswahili kwa kutoa mifano.
3. Eleza athari ya majilio ya wageni katika Kiswahili, ukitoa mifano.
4. Ukoloni wa Ujerumani ulisaidiaje katika kukuza Kiswahili?
5. Wamisionari walikuzaje Kiswahili? Eleza.
6. Krapf alikua na matatizo gani katika Kiswahili? Toa mifano.
7. Kwa nini Krapf anakumbukwa katika historia ya Kiswahili? Eleza.
8. "Inter-Territorial Language Committee" ni nini na ili fanya kazi gani?
9. Kwa nini Rwanda imeamua kufundisha Kiswahili Sanifu?

SURA YA PILI: FASIHI

Fasihi ni nini?

Fasihi ni kazi ya sanaa imulikayo hisi, mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha. Fasihi ni sanaa ya matumizi ya maneno kisanaa. Hakuna maneno ya kisanaa, bali maneno haya haya ya kawaida hutumiwa kisanaa na msanii.

Hapa tutapata swali lingine:

Sanaa ni nini?

Sanaa ina uzuri! Kila kazi ya sanaa ina uzuri wa aina yake, ambao unakusudiwa kutolewa na msanii. Uzuri huo waweza kuonekana, kusikiwa, kuguswa au kuonjwa ikitegemea aina ya sanaa.

Lakini sanaa si uzuri tu, hubeba ujumbe au maudhui maalumu kwa jamii. Hivi ndani ya sanaa kuna ujumbe. Huo ujumbe unaweza ukapatikana kwa urahisi au kwa taabu kutegemea jinsi ujumbe ulivyotolewa na kwa kutegemea aina ya sanaa, pia hutegemea uwezo wa mchambuzi wa hiyo sanaa katika kupata ujumbe.

Sanaa pia ina tabia ya kutoa upya. Kazi ya sanaa si nakala ya kazi nyingine, bali ni kiumbe kipya kabisa akiumbacho msanii.

DHIMA YA FASIHI

Fasihi huhusika au hujishughulisha na nini maishani? Fasihi hujishughulisha na ubinadamu na mazingira yake ya kila siku. Fasihi hueleza hisi za binadamu kwa njia ya maneno kwa yote anayoyahisi, anayoyasikia, anayoyaonja, yanayomgusa na yanayomkabili. Si hayo tu, bali mambo ya ndani ya nafsi yahusuyo imani na itikadi.

Kwa kuwa fasihi hushughulikia ubinadamu na ubinadamu ni mpana, wenye urefu na kina kirefu sana; basi fasihi nayo ni pana, ndefu na ina kina kirefu sana.

Hakuna binadamu awezaye kuelezea ubiadamu wote maishani. Msanii ambaye ni binadamu aweza kueleza sehemu moja ya ubinadamu lakini si ubinadamu wote. Ndiyo maana tunasema kuwa hakuna msanii awezaye kudai kuwa amemaliza kusema yote katika fasihi.

Fasihi kama sanaa hutumia lugha yaani maneno, na lugha ni sehemu ya utamaduni, ni chombo cha kueleza na kuhifadhia utamaduni.

Fasihi leo hugawanyika katika nyanja au taaluma mbili kuu, yaani **fasihi simulizi** na **fasihi andishi**.

1. FASIHI SIMULIZI

Fasihi simulizi ni fasihi, maana nayo ni sanaa ya maneno yenye uzuri, upya na ujumbe. Wengi wamepambana na “fasihi andishi” maana vitabu vingi vimetolewa na vinaendelea kutolewa katika fani au tanzu hii. Wala hatusemi kuwa **fasihi simulizi** ni somo geni au hakuna vitabu vilivyoandikwa juu yake, vipo vitabu vilivyoandikwa juu yake; lakini si vingi kama vya fasihi andishi.

Fasihi simulizi ni masimulizi ambayo kwa asili hayakuandikwa wala kunaswa katika vinasia sauti, japo leo jitihada iliyopo ni kuhifadhi hayo mapokeo ya masimulizi katika maandishi na kanda za kunasia sauti fasihi. Simulizi ni masimulizi juu ya mambo ya kale na yenye misingi ya mila au tamaduni za jamii.



Pamoja na ukale wake, fasihi simulizi bado inaendelea katika “Uleo” wa karne hizi katika jamii ya sasa. Kuna masimulizi mengi leo hayajaandikwa na mambo ya asili katika tamaduni za jamii zetu.

Fasihi simulizi ni kiungo kati ya kale na leo. Hufufua ya kale na kuyaleta ya leo na kuyapa maana katika maisha ya leo. Hutuletea falsafa ya kale na kuturithisha hayo katika kizazi cha leo. Huibusha sanaa ya kale na kuitajirisha sanaa ya leo. Huchimbua historia ya leo. Hutuonyesha tulikotoka na kueleza asili yetu ili tujivunie.

Fasihi simulizi huunga jana na leo yaani kale na siku hizi. Umuhimu wake hujitokeza katika tanzu zake mbalimbali.

1.1. TANZU ZA FASIHI SIMULIZI

i) Hadithi

Hadithi ni mambo ya kubuni ambayo huwa yanaeleza ukweli fulani katika jamii. Kwa maelezo haya, hadithi kwa asili yake ni habari ambayo inasimuliwa. Hadithi ina mtindo wake wa kusimuliwa.

Kwa mfano:

Mwanzoni

1. **Msimulizi:** Paukwa! (2)

Wasikilizaji: Pakawa! (2)

Msimulizi: Hapo zamani za kalepalikuwepo

2. **Msimulizi:** Hadithi! Hadithi! (2)

Wasikilizaji: Hadithi njoo! (2)

Hapo zamani

Mwishoni

- Huu ndio mwisho wa hadithi

- Hadithi inakomea hapa



Maneno haya hutumiwa kama umuhimu ufuatao:

- Kuvuta na kuwaamusha wasikikilizaji
- Kuwaweka katika muktadha

Vipera vya hadithi

a) Ngano

Ni hadithi fupi ambazo zinazosimuliwa ili kuwasaidia watoto kupata maarifa mbalimbali kwenye maadili ya jamii.

Wakati mwingine ngano huambatana na nyimbo. Wahusika wa ngano ni wa aina nyingi, yaani mchanganyiko: **binadamu, mizimu, miungu, wadudu, wanyama, n.k.**

Pia vitu visivyo na uhai hutumiwa kama wahusika kama vile **mawe, milima, miti, n.k.**

b) Hurafa

Ni hadithi ambazo wahusika wake ni **wanyama** ingawa wanyama wenyewe kwa kawaida huwa na tabia za kibinadamu. Ni aina moja ya hadithi ambayo imeenea sana karibu Afrika nzima.

c) Hekaya

Hekaya kwa kawaida ni kisa kifupi kilichokusudiwa kubaini hekima au funzo fulani. Kwa mfano: Yesu alikuwa akitumia sana hekaya katika mafunzo yake ya kila siku.

Hekaya zina wahusika ambao ni **binadamu tu**. Hekaya ambazo zinajulikana sana Uswahilini ni za Abunuwasi.

Mfano wa hadithi

KOBE NA NYANI

Kobe na Nyani waliolewa katika kijiji kimoja. Nyani alikuwa na shughuli ya kukata miti katika shamba lake. Alimwomba Kobe amsaidie ili shamba lisafishwe upesi kuwahi majira. Kobe aliitikia wito na siku waliyopatana ilipowadia wote walikuwa katika shamba la Nyani na mashoka yao.



Kazi ilipamba moto. Upande aliosimama mzee kobe miti iliangamia kama mchezo tu. Upande wa Nyani haukuonyesha maendeleo makubwa.

Nyani alianza kulalamika.

‘Mzee Kobe, naona leo shoka langu linarudisha nyuma juhudi yangu. Niliona karibu asubuhi yote ya jana lakini bado linaonekana kuwa ni butu’.

Mzee Kobe akasema.

‘Kama ni hivyo ngoja ni kuazime langu, maana mimi nipo karibu kumaliza hii sehemu uliyonipimia. Nitajikokota na shoka lako butu’.

Basi jamaa hao wawili walibadilishana mashoka. Nyani alikata miti kwa shoka la Kobe sasa. Miti ililazwa pasipo kifani. Nyani alilipenda shoka lile na mwisho wa kazi yao alimwambia mzee Kobe.

‘Mzee Kobe, hili shoka ni kali na jepesi sana katika kukata miti. Kwa sifa hizo ninaomba uniazime ili kesho nitakapokwenda kukata miti katika shamba la mkwe wangu nilitumie. Maana bila ya hivyo nitaonekana mvivu’.

Mzee Kobe alimruhusu Nyani abaki na shoka lake, lakini kwa sharti kwamba lazima alirudishe mara ya kumaliza kazi yake. Baada ya hapo walikula chakula ambacho kililetwa na mke wa Nyani, wakaagana na kila mmoja akaelekea kwake.

Baada ya siku ile, siku nyingi zilipita bila ya Nyani kuonyesha dalili yoyoyte ya kurudisha shoka la mzee Kobe. Siku moja Kobe aliamua kwenda nyumbani kwake. Alipofika kule Nyani alimkaribisha Kobe harakaharaka.

‘Rafiki yangu mpenzi, karibu sana, najua shida iliyokuleta hapa. Kaa kitako tulegeze makoo kwa pombe kidogo ambayo alitengeneza mke wangu’.

Mzee Kobe alihisi kwamba kulikuwa na njama ya aina fulani. Baada ya kunywa pombe hiyo kidogo bwana Nyani alitoa kauli ifuatayo.

‘Rafiki yangu Kobe. Ninasikitika kukuarifu kwamba lile shoka lako hutalipata tena. Nilimwazima mjomba naye kaniarifu kuwa hivi majuzi tu mwizi aliivamia nyumba yake akaliiba. Kwa hayo yote nasema pole sana’.



Mzee Kobe hakutoa kauli yoyote. Aliondoka akarudi zake nyumbani. Siku nyingi zilipita na habari za shoka zilikwisha kusahaulika. Siku moja Kobe alimwita mkewe akamweleza.

‘Mke wangu, unikatekate katika vipande vipande halafu nyama yangu iwe kitoweleo kizuri kabisa. Baada ya hapo pika chakula halafu ukakiweke katika njia panda. Hakikisha unafanya hivyo wakati Nyani yumo shambani mwake’.

Mkewe hakukubaliana na mawazo yake; lakini Kobe alisisitiza na alimwondoa hofu kwamba kitendo kile hakingekuwa na madhara.

Baada ya mabishano makali mkewe Kobe alifanya kama alivyoelekezwa na mumewe. Alimkatakata mumewe vipande. Nyama yake akaikaanga vizuri sana. Akatengeneza wali. Chakula kilipokuwa tayari, alikifunika na kukipeleka njia panda karibu na shamba la Nyani. Bahati njema Nyani alikuwemo shambani mwake siku ile. Alikuwa amekwisha kufanya kazi kwa muda mrefu na sasa alijisikia ana njaa. Aliamua kuweka shoka lake begani na mara akaanza safari ya kurudi nyumbani.

Alipofika njia panda alianza kuhisi riha nzuri ya chakula. Mate yalianza kumdongoka Nyani, naye hakuchukua muda kugundua kwamba kulikuwa na chakula hicho mahali pale. Bila kujiuliza aliyekwenda kukiweka pale, akaanza kukishambulia.

‘Uhuru ruruu! Ngururuu! Ngururuu!’

Nyani alishangaa.

‘He! Mabo gani tena haya! Badala ya kuwa ninapiga mbeu ya shibe, tumbo linanguruma!’

Akiwa katika mshangao huo alisikia sauti kutoka tumboni mwake.

‘Unashangaa nini! Usishangae. Mimi ninataka unirudishie shoka langu.’

Nyani aliona mambo yamekuwa makubwa. Alianza kuharakisha kwenda nyumbani.

Hofu ilimshika. Ilikuwa shani yenye kashifa ndani yake. Alijua wazi mzee Kobe alimcheza shere. Alikuwa amenuia kumwadhiri kwa kisasi cha kudhulumiwa shoka

lake. Alipofika nyumbani alionekana kuwa na wasiwasi sana. Mkeke alimtayarishia chakula lakini hakuwa na hamu ya kula.

Tumbo lilinguruma tena na sauti ilisikika kutoka tumboni,

‘Mimi sina ugomvi nawe. Ninataka shoka langutu basi. Nenda kalitupe pale njia panda ulipokikuta chakula ulichokula’.

Nyani kusikia hivyo alikurupuka akaenda kuchukua shoka alipolificha na wakati huo alielekea njia panda.

Alilitupa shoka la mzee Kobe pale. Kitambo kidogo baada ya hapo alijihisi ameshikwa na na haja kubwa. Alichepuka kando ili ajisaidie. Katika kujikwinya alijihisi kama kulikuwa na kitu kigumu katika matumbo yake. Mwishoni alimnya mzee Kobe, nusura apasuke msamba mzee Kobe alipodondoka gamba lake likapasuka likawa na nyufanyufa. Kisha akachukua shoka lake. Mzee akaenda nyumbani taratibu kwa maumivu.

Mkeke Kobe alimpaka dawa akapona. Hata hivyo mistari dabo ipo hata leo.

Na huo ndio mwisho wa hadithi.

ZOEZI

1. Nyani alimfanyia hila gani Kobe?
2. Kobe alifanya nini ili kupata shoka lake?
3. Je, tabia ya Nyani inakubalika katika jamii?
4. Umepata funzo gani kutokana na hadithi hii.

ii) Vitendawili na mafumbo.

Vitendawili ni maneno yanayotumia lugha ya mafumbo na huitaji ufumbuzi au majibu. Vitendawili ni sanaa pevu na huwa na usanii wa daraja la juu unaohitaji uwezo wa kujibu kiufundi na kimvuto. Hali hii hutaka ujuzi mkubwa kulingana na tamaduni za mazingira ya jamii inayohusika. Kitendawili kinaweza kuwa na undani ambao ni nadra kuupata.

Katika jamii nyingi za kiafrika, vitendawili viliweza kutegwa na kuteguliwa jioni wakati wa kupumzika baada ya shughuli za kazi za mchana kutwa. Kila kitendawili huzungumzia swala fulani na hivyo huwa na **maudhui** na **fani**.

Vitendawili huzingatia mfumo fulani wa kutega na kutegua. Miongoni mwa Wabantu kulikuwa na utaratibu unaokaribiana kama ufuatao:

. **Kitangulizi (mtegaji):** Kitendawili

(mteguaji): Tega

. **Kitendawili chenyewe (mtegaji)**

. **Jibu (mteguaji)**

Kitendawili kikikosa kuteguliwa mara mbili, tatu au zaidi mji au kichocheo hutolewa na wateguzi baada ya mtegaji kuomba kupewa mji. Kisha anapewa mji.

Mifano ya vitedawili:

- | | |
|------------------------|---|
| 1. Kitendawili: "Tega" | Kipo lakini sikioni. Kisogo |
| 2. Kitendawili: "Tega" | Kombe la Mungu li wazi. Kisiwa |
| 3. Kitendawili: "Tega" | Nzi hatui juu ya damu ya Simba. Moto |
| 4. Kitendawili: "Tega" | Nyumba yangu kuu ina mlango mdogo. Chupa |
| 5. Kitendawili: "Tega" | Nina watoto wane lakini akiondoka mmoja waliosalia hawafanyi kazi. Matendegu ya kitanda au magurudumu ya gari. |
| 6. Kitendawili: "Tega" | Mgeni akifika anakuta askari mwenyeji naye akirudi anakuta askari yuleyule anasimama. Kufuli ya mlango. |
| 7. Kitendawili: "Tega" | Mlima wa kwetu una msitu mweusi juu. Nywele za mtu mweusi. |

Mafumbo ni kauli zinazoeleza jambo kwa njia isiyo wazi. Mafumbo hutumia taswira (picha) ili kuwafikisha wasikilizaji katika ufumbuzi. Mafumbo huwa na kianzio kifuatacho:

(msimulizi): “Fumbo mfumbie mjinga”

(msikilizaji): “Mwelevu huling’amua” (alfumbue).

Mfano:

Watu watatu walikuwa safarini walipofika mtoni iliwabidi wote watatu kuvuka kwenda ng’ambo lakini hawakuwa na mashuwa wala daraja la kuvukia. Wakati wa kuvuka mmoja aliyaona na kuyakanyaga maji, mwingine aliyaona na hakuyakanyaga maji naye, watatu hakuyaona wala kuyakanyaga lakini alivuka. Je, walikuwa nani?

Ufumbuzi:

- Aliyeyaona na kuyakanyaga ni Mama mjamzito
- Aliyeyaona pasi na kuyakanyaga ni mtoto aliyebebwa mgongoni
- Aliyekosa kuyaona na kuyakanyaga ni mtoto aliyekuwa tumboni mwa mama yake.

iii) Nyimbo na ushairi

Wimbo ni maneno yaliyopangwa yakiwa na ujumbe maalumu na kutamkwa kwa sauti ya mziki. Wimbo huwa na mdundo unaosisimua na mara nyingine kunakuwepo na mlingano wa sauti katika miisho ya maneno. Kuna nyimbo ambazo hufuatana na zana za mziki, kama marimba, zeze, ngoma, zumari, nanga na zana nyingine. Zana hizo hufanya nyimbo zisisimue zaidi. Kuna nyimbo ambazo hazitumii zana kabisa, hutumia sauti tu. Hizo zote ni nyimbo.

Afrika ni Afrika iimbayo. Afrika ni tajiri sana katika uimbaji. Afrika yetu watu wake huimba katika shughuli mbalimbali na mahali mbalimbali na wakati mbalimbali. Toka motto azaliwe husikia nyimbo mpaka dakika ya mwisho ya maisha yake Mwafrika husikia nyimbo.

Nyimbo huwa katika tamasha (sherehe) nyingi kwa makusudi mbalimbali kama tulivyosema. Kuna nyimbo kwa mfano za kubembeleza mtoto. Mtoto aliapo, mama humbembeleza hadi alalapo. Aweza akambembeleza maana saa za kulala zimetimia au kwa sababu mama ana kazi. Kuna nyimbo nyingi katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Nyimbo hizi zimeenea katika maisha ya Waswahili na huwafuata tangu wanapozaliwa mpaka kufa kwao. Nyimbo hizi kwa kawaida huwa zimefungamana na ngoma au michezo fulani na mara nyingine huimbwa pamoja na mziki.



Aina za nyimbo

1. Nyimbo za watoto
2. Mbembelezi
3. Nyimbo za sherehe (kutahiri, arusi, mavuno, maulidi, n.k.)
4. Taarab

Nyimbo ndizo zinazozaa ushairi katika jamii nyingi katika Afrika. Hii ndiyo maana nyimbo na ushairi tunaviambatanisha pamoja.

Ushairi ni uimbaji, na shairi ni wimbo, lakini si kila shairi huimbwa au huimbika. Yapo mashairi ambayo huimbwa na mengine ya kukuriri tu. Kutoka kwenye nyimbo, mashairi yamesanifiwa na kuwa ni tanzu ya pekee yenye sanaa ya juu ya lugha, hasa ushairi wa Kiswahili.

iv) Methali

Methali ni lugha ya mifano ambayo huwa na makusudi ya kutoa mafundisho, maadili, kuonya, kufumba kwa kutumia maneno machache. Methali ni misemo yenye hekima fulani. Methali hudhihirisha mkusanyiko wa mafunzo waliyopata watu wa vizazi vingi vya jumuiya fulani katika maisha yao. Ni sehemu moja ya lugha inayoweza kubaini falsafa ya watu fulani kuhusu maisha kwa ujumla.

Methali inadhihirisha mambo mawili:

- a) Ni njia ya kufumba na kupigia mfano
- b) Ina maana pana na maneno ya kisanii.

Waandishi wengine wanasema kwamba methali ni semi zenye busara zitoazo maadili mbalimbali katika maisha ya mwanadamu, semi zenye kueleza kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili kutoa maadili au onyo fulani.

Methali imeundwa na kutolewa kulingana na mawazo kadhaa na nia maalumu kwa faida ya jamii. Mawazo yaliyomo ndani ya methali yanashikamana na tamaduni, desturi na hadhi ya jamii hiyo husika. Methali hutumiwa sana katika mazungumzo ya kawaida ya Waswahili.

Mifano ya methali:

- Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
- Bibi mzuri hakosi kilema.
- Chema hakidumu.
- Heri nusu ya shari kuliko shari kamili.
- Jinga ni lako mwenyewe, la mwenzio huwezi kuitumia.
- Karamu mbili zilimshinda fisi.
- Kidole kimoja hakivunji chawa.

v) Nahau

Nahau ni semi fupi zinazotofautina na maana yake ya asili. Nahau hutumia picha na kutoa maana kamili katika maisha. Ni kauli zilizojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini zinatoa maana isiyo ya kawaida, yaani maana fiche.

Kwa wajifunzao lugha hii ya Kiswahili; kuweza kuzielewa nahau sawa sawa na kuweza kuzitumia vizuri kwa ufasaha ni kuonyesha mtu amepvuka katika lugha hii. Nahau si ngumu lakini thamani yake ni kuwa nahau mara nyingi mtumiaji wa Kiswahili huzitumia sana bila kujua kama anazitumia katika mazungumzo.

Maana za nahau huwa kamili na ni mara chache nahau moja iwe na maana zaidi ya moja, labda tu ilazimishwe katika matumizi.

Semi hizi huambatisha kitenzi na nomino (K+N).

Mifano:

- Kupata jiko= Kuo
- Kupata kileo= Kulewa sana
- Kupasuka moyo= Kushtuka
- Kupasua bomu= Kusema jambo la fedheha (kukasilisha)
- Kukata kiu= Kupata kinywaji

- Kukata maini= Kuudhi mtu (kuumiza mtu moyoni)
- Kukata nakshi= Kutia urembo
- Kutia kifua= Kufanya jambo kwa pupa (bidii)
- Kutia jeki= Kuinua au kusaidia mtu
- Kutia kapuni= Kupuuzua au kusahau jambo

vi) Majigambo

Majigambo ni utanzu wa fasihi simulizi ambayo yana uhusiano wa karibu na mashairi. Dhana ya kujisifu ndiyo ambayohuwa dhamira kuu ya majigambo.

Majigambo yanahusiana na kujitangazia sifa, kujitakasa kuwa una makosa ambayo ni kujinaki. Tena kujigamba na kujinata (yaani kujiona bora kuliko watu wengine) au kujiketua (yaani kujifanya kuwa na mambo usiyokuwa nayo).

vii) Miiko/Mizio

Kwa kawaida mzio au mwiko ni jambo au kitu kinachozuiwa mtu kutumia kwa kuogopa kupata madhara. Mzio ni jambo ambalo mtu hawezi kulitenda kwa sababu ya tabia mazoea au imani.

Mzio ni hali ya kutoweza kula kwa sababu ya kuchelea kudhurika. Miiko imejengwa kupiitia misemombalimbali kama vile:

- **“Ni mwiko au mzio ku.....”**

Pengine unaweza kusema **”kufanya hivi na hivi ni.....”**

- **“Inakatazwa kufanya..... ”**

Mifano:

- Kufagia usiku kunakimbiza baraka.
- Mwenye kula miguu ya kuu atakuwa daima katika mwendo.
- Inakatazwa kunywa maji ndani ya kata pasi na kuikung’uta.
- Kushona nguo mwilini kunaleta ufukara.
- Mwenye kufanya mazoea ya kukaa kizingitini atakawia kuo.

2. FASIHI ANDISHI

Fasihi andishi ukilinganisha na fasihi simulizi, katika jamii nyingi za Kiafrika, hii ndiyo fasihi changa, wakati fasihi simulizi ni ya kale zaidi.

Fasihi andishi kwetu ilianza wakati tulipoanza kuweka amali zetu za jamii katika maandishi hasa wakati tulipoanza kutumia maandishi kuhifadha historian a tamaduni zetu.

Katika Afrika ya Mashariki na ya Kati fani ya uandishi iliingizwa na wageni zaidi. Upo ushahidi kuwa wazee wetu walianza kuhifadhi fikra zao michoro mapengoni. Sanaa hiyo ya michoro haikuendelezwa. Mataifa mengine yaliendeleza michoro yao na kuwa na maandishi yao kwa mfano, Wachina na Wajapani.

Wageni waliotujilia ni Wachina, Wareno, Waarabu, Wadachi na Waingereza. Wengi wa hao hawakuweka athari ya kielimu; hivi wale waliowahi kuweka athari ya elimu ndio waliokuwa waanzilishi wa kutuletea maandiko. Tunalotaka kusema ni kuwa hati ambazo zimeletwa na kwetu Afrika ya Mashariki na Kati ni hati ya Kiarabu, Kilatini, Kiebrania na Kiyunani. Kiebrania na Kiunani hazikuleta athari sana kwa watu, ila hati ya Kiarabu na hati ya Kilatini ndizo zilizomiliki. Kiarabu kilianza na hatimaye pole pole Kiswahili kikabeba hati ya Kilatini ambayo ilitumika na Wadachi na Waingereza.

Fasihi andishi katika jamii zetu ni somo changa lililoanza na hati ya Kiarabu na kukuomaa katika hati ya Kilatini.

2.1. TANZU ZA FASIHI ANDISHI

Fasihi andishi inazingatia tanzu mbalimbali ambazo ni;

- Hadithi: a) Hadithi fupi
 b) Riwaya
- Tamthiliya: a) Ramsa
 b) Tanzania
 c) Tanzania-Ramsa
- Ushairi: a) Mashairi
 b) Tenzi
 c) Ngonjera

1. HADITHI:

A) HADITHI FUPI: hizi huwa ni hadithi za kubuni kutoka katika mazingira ambazo huhusishwa na matukio au mambo mbalimbali katika maisha ya watu ya kila siku.

Hadithi hizi hukusudiwa zaidi kuliko kusimiliwa.

Hadithi fupi, kwa umbo huwa fupi, kwa kila kipengele kuliko riwaya. Hadithi fupi huwa na maneno kiasi ya 30,000.

1.1. Fani katika hadithi

Katika kiwango hiki, tutazingatia mambo mbalimbali ya msingi katika kukabili kazi ya fasihi andishi au kazi yoyote ya kifasihi. Japokuwa hapa tutaingia zaidi katika kuitazama fani katika hadithi.

Kimsingi fani na maudhui hukamilishana, kwa sababu ujenzi wa fani huathiri moja kwa moja jinsi maudhui yanavyotolewa. Itokeapo kwamba fani inalegalega, basi hata maudhui itakuwa vigumu kuyafikisha yalivyokusudiwa. Hali kadhalika, upo umuhimu mkubwa kwa maudhui kuwepo katika fani bora. Vile vile tutaangalia jinsi vipengele mbalimbali vya fani vinavyoweza kuleta athari mbalimbali katika hadithi.

Katika utanzu wa hadithi, fani yake huzingatia mambo mbalimbali yakiwemo lugha, mandhari, mtindo, mtiririko wa visa (muundo) na mengineyo ambayo tutayaangalia kiundani zaidi hapa na hasa kuona vipengele hivyo jinsi vinavyotegemeana na kuhusiana katika kuunda na kukamilisha fani ya hadithi za Kiswahili.

1.1.1. Wahusika

- Jinsi wahusika hao wanavyojengwa na
- Jinsi wanavyojitokeza katika kazi ya sanaa inayohusika.

Wahusika huwa ni watu, wanyama, vitu au viumbe wa kufikirika. Mwandishi wa hadithi, huwajenga wahusika wake kisanaa ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za uhalisi wa maisha katika jamii.

Kwa hiyo, mwandishi wa hadithi au kazi yoyote ya fasihi hukabiliwa na kazi kubwa ya kuwaonyesha wasomaji wake jinsi wahusika wake walivyo; iwapo ni watu kwa

kuwatambulisha na sifa zao; mambo wanayoyapendelea, nay ale wasiyoyapenda, jinsi walivyo, wanavyokabili maisha, n.k. Matumizi ya lugha ya wahusika hao pia huwa muhimu. Jinsi wahusika wanavyotumia vipengele mbalimbali vya lugha kwa tamathali za usemi, misemo mbalimbali, nahau, methali, n.k.

Baadhi ya wasanii, wameamua kuwapa wahusika wao majina yanayoelezea tabia zao. Msanii maarufu katika kutumia mbinu hii katika uandishi wa Kiswahili ni Shaban Robert, ambaye hutumia majina ya: Hisidi kwa mtu hasidi, Adili kwa mtu adili, Mwivu kwa mtu mwenye tabia ya wivu, Busara kwa mtu mwenye busara. Hata mahali ambapo matukio ya hadithi yanatokea, kwa sababu ni pa kufikirika tu, anapaita Ughaibu, kufikirika n.k.

Namna nyingine ni ile ya msanii kuwaelezea yeye mwenyewe jinsi walivyo.

“Karake alikuwa mtu mwenye roho iliyotakata, roho iliyompenda kila mmoja kikijini pao. Maneno yaliyokuwa yanataka ulimini mwake yaliwapendeza wote, licha ya kuwa na busara yeye hakuchagua hirimu ya watu.....”

Namna nyingine ni ile ya kuwaumba wahusika kutokana na matendo yao katika hadithi. Jinsi wanavyotenda, wanavyosema, wanavyowaza, maumbile yao na kadhalika.

Kutokana na ujengaji wa wahusika wa namna hii, msomaji anaweza kumwona mhusika akionyesha wasifu wake wa ndani na nje au anaweza kuonyesha mabadiliko yake.

Wakati mwingine ikibidi, mwandishi anaweza kumjenga mhusika mmoja kwa njia ambayo ni tofauti na wahusika wengine katika kazi yake kwa makusudi ili aweze kujenga dhamira aliyokusudia.

Msanii anaweza kuwawasilisha wahusika katika udhahiri. Katika mbinu hii sifa na matendo ya ya mhusika yanaelezwa waziwazi. Msomaji akishasoma hadithi inayohusika anaweza kumwelewa sana mhusika huyo.

Njia hii ya uumbaji wahusika husaidia kumfanya msomaji asipate taabu katika kutambua kiini cha kisa, wazo au dhamira, msanii hapa anamjenga na kumtumia mhusika huyo kutoka mwanzo hadi mwishoni mwa hadithi yake.



1.1.1.1. Makundi ya wahusika

Katika hadithi, tunaweza kuwagawa wahusika katika makundi matatu muhimu ambayo kwayo hutumiwa na mwandishi kutolea dhamira zake. Makundi hayo ni ya wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi.

a) Wahusika wakuu

wahusika hao, ambao kwa kawaida ni mmoja au wawili hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Mara kwa mara wahusika hawa hubeba kiini cha dhamira kuu na maana ya hadithi yote katika wahusika wa hadithi za tanzia, wahusika wengi huonyesha mabadiliko mengi kama vile anguko pia mhusika hufikia kilele na mwisho akaanguka. Pengine mhusika anaweza kuonekana anapanda na kuwa mashuhuri, na halafu akakuwa duni katika hadithi.

Wahusika wakuu wanaweza kuwakilisha vikundi, jamii au mtu binafsi.

b) Wahusika wajenzi

Mbali na wahusika wakuu kuna wahusika wajenzi. Wahusika hao ni muhimu sana kama walivyo wahusika wakuu katika kazi ya sanaa. Wakati mwingine wahusika wa aina hii hujengwa sambamba na wahusika wakuu katika juhudi ya kuwajenga na kuwafafanua vizuri zaidi wahusika wakuu. Kuweco kwa wahusika hao kunasaidia sana kuipa hadithi ama kazi nyingine ya sanaa mwelekeo muhimu wa kisanaa na maudhui. Wahusika hao wana tabia ya kujitokeza mara moja moja. Kwa jumla wahusika wote hawa wana tabia ya kuhusiana na kutegemeana. Wanasaidia kukuza, kudumaza ama kufanya maamuzi muhimu ya hadithini.

1.1.1.2. Tabia za wahusika

Katika makundi mawili ya wahusika tuliowaona hapa juu, tunaweza kupata tabia za wahusika za aina tatu. Tabia hizo ni za **ubapa**, **uduara** na **ufoili**.

- i) **Ubapa:** ubapa huwakilisha aina moja tu ya tabiakutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Toka mwanzo hadi mwisho tabia hii inajidhihirisha katika mhusika anayeishi katika wazo na sifa za aina moja bila kubadilishwa na wakati, mazingira, uhusiano wao na wengine, n.k. Tabia hiyo haibadiliki kufuatana na hali za

kawaida za maisha ya binadamu zinazobadilika kihistoria. Tabia hii inaelezwa kwa kutumia wahusika bapa-sugu na wahusika bapa vielelezo.

Wahusika bapa-sugu ni wale ambao wanaonyesha msimamo wao kutokana na maelezo ya msanii. Wanakuwa sugu katika maana kwamba hawabadiliki, kila wanapoonekana hali zao huwa ni zile zile, hawahukumiwi bali huhukumu tu, hawaongozwi bali huongoza tu.

Wahusika bapa-vielelezo kwa upande mwingine ni wale ambao pamoja na kutobadilika kwao, wanapewa majina ambayo humfanya msomaji aielewe tabia na matendo ya mhusika huyo.

Katika hali hii ya wahusika, msanii anatilia mkazo wake katika aina moja ya tabia inayotawala, na ambao iwafikie wasomaji kiasi ambacho sehemu zote za sifa za mhusika huyo hazitokezi. Aidha, wahusika bapa hawawakilishi hali halisi ya tabia za watu wanaoishi, kwa kawaida huonyesha kipengele kimoja tu cha tabia hata kama wanakutana na mazingira mbalimbali.

ii) Uduara: uduara ni tabia ambayo mhusika mmoja hujenga akionyesha tabia tofauti. Tabia ya uduara humfanya mhusika kubadilikabadilika kihulka, kimawazo na kisaikolojia.

Wahusika wenye tabia hiyo huonyesha kubadilika ambako kunatokana na mazingira mapya. Sifa kuu ya wahusika wenye tabia hiyo, hadithini huishi maisha kawaida yanayofanana sana na jamii kiasi ambacho msomaji huwakubali kuwa ni wahusika hai.

iii) Ufoili: ufoili ni tabia inayojidhihirisha kati ya wahusika duara na wahusika bapa. Lakini pia ni tabia inayoonyesha hali zaidi kuliko wahusika bapa. Ili waweze kujengeka vyema, wahusika wenye tabia hii huwategemea sana wahusika duara na wahusika bapa. Kwa hiyo, wahusika wenye tabia ya ufoili wana msukumo wa nafsi ulio tofauti na wahusika wakuu ama wahusika wengine muhimu katika kazi ya sanaa.

B) RIWAYA: riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, ambayo huwa inakusudia kuifikia hadhira kwa kupitia njia ya maandishi. Riwaya aghalabu huwa na maneno yanayozidi 30,000. Riwaya ina dhamira zake, wahusika, muundo wake na mtindo wa aina yake.

Lugha itumikayo katika riwaya ni aina ya nathari (maandishi ya moja kwa moja, maandishi ya kawaida) na hutumia mchanganyiko wa vipengele vya lugha kama vile tamathali za usemi, methali, nahau, mafumbo, kejeli, ishara, n.k. Kwa sababu ya urefu wake, hifadhi yake huwa katika maandishi. Tusomapo riwaya tunatalii maisha ya binadamu, wanyama, na amali zote za jamii.

B.1. Aina za riwaya

Kuna riwaya za aina nyingi. Kuna riwaya za mapenzi, upelelezi, kisiasa, kidini, kihistoria, n.k.

B.2. Mambo ambayo hujenga riwaya

- i) **Maudhui:** Yale ya maana ambayo tunayapata kutokana na riwaya baada ya kuisoma. Dhamira zote na ujumbe tunaobaki nao.
- ii) **Fani:** Jinsi riwaya ilivyojengeka. Lugha ya mjazo ndicho chombo cha kuibushia maudhui. Riwaya huwa na mtiririko wa vituko. Jinsi tukio moja linavyoathiri jingine ndivyo riwaya inavyosukumwa mbele. Riwaya vilevile huwa na upeo wake. Hapa ndipo hisia za msomaji zinapovutwa na tunapata mchomo kiasi cha haja yetu kukidhiwa. Mandhari ya riwaya ni ya aina nyingi. Matukio hutendeka katika sehemu mbalimbali za nchi na mwandishi huranda sehemu zote hizo akitupeleka wasomaji katika riwaya yake. Mwisho wa riwaya ndipo msomaji hutazamia ufumbuzi wa maswala yaliyoibushwa. Kuna riwaya ambazo huwaacha wasomaji wakielea na kuwafanya wafikiri katika kutafuta suluhisho. Riwaya huweza kuchukua mitindo mbalimbali. Kwa mfano, kuna ambazo mwisho huwa mwanzo na mwanzo huwa mwisho.
- iii) **Wahusika:** Wahusika katika kazi ya sanaa itumiayo lugha huweza kuwa watu, wanyama au viumbe vinginevyo. Wahusika katika riwaya si watu au viumbe halisi, bali ni mkusanyiko wa tabia kutoka kwa watu au viumbe halisi wanaoishi au walioishi. Madhumuni ya kuwaumba watu hao ni kuwakilisha dhana mbalimbali na kutoa ujumbe kwa jamii kama msanii anavyotaka. Mwandishi huonyesha sifa zao, hali yao, na maisha yao kwa ujumla katika ulimwengu waishimo. Watazungumza wakitumia vipengee mbalimbali vya lugha kama methali, nahau, misemo, tamathali za usemi, n.k.

Mwandishi anaweza kuwaeleza sifa za wahusika wake kwa kuwapa majina yenye sifa anazotaka kuwapa au anaweza kuwaelezea yeye mwenyewe walivyo kutokana na matendo yao, mawazo yao na maumbile yao. Ufuatao ni mfano wa uumbaji wa mhusika unaoangukia katika mtindo huo wa pili.

“... Rosa alikuwa mzuri, mrefu kiasi, mnyenyekevu na mnyamavu. Kama akienda kuoga kisimani utamwona kabla ya kuvua nguo anaanza kuangalia huku na huko, huvua, huoga upesi, huvaa, huchukua maji na kurudi nyumbani. Akifika nyumbani anajikuta bado ana mapovu ya sabuni sikioni. Alikuwa hapendi kuangaliwa kwa muda mrefu. Ukimwalia machoni huinamisha kichwa.....”

iv) Aina za wahusika:

- **Wahusika wakuu:** Hawa hujitokeza tangu mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Aghalabu hubeba kiini cha dhamira na maana ya hadithi yote. Matukio katika riwaya hujengwa yakiwazunguka wao. Wahusika hawa huweza kuwakilisha vikundi, jamii au mtu binafsi.
- **Wahusika wadogo:** Huwasaidia wahusika wakuu katika kusukuma migogoro ya hadithi mbele na kutoa maudhui. Wahusika wadogo huibuka wakati fulani fulani tu.

Aina hizo mbili za wahusika huweza kuwa wahusika bapa au la. Wakati wahusika ni bapa, huwakilisha aina moja tu ya tabia kutoka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Hawaathiriki na wakati, mazingira na mahusiano yao na wengine katika tabia zao. Wahusika bapa huwa ni kiwakilisho thabiti cha msanii katika kutimiza lengo fulani licha ya hali za kawaida za maisha ya binadamu ambao hubadilika kadiri wakati unavyopita.

Wahusika bapa hutambulika kwa tabia yao ya kuhukumu tu, kutoshairika, kupenda kuongoza tu, n.k. Pamoja na hali hizo za hapo juu, hupewa majina ambayo husadifu tabia zao. Hasa tabia ile inayomtawala mhusika, ambayo mwandishi angependa waione wasomaji. Hivyo, kama mhusika anatawaliwa na tabia ya kujivuna ataitwa Majivuno, kama ni mbinafsi ataitwa Boramini, n.k.

Kundi jingine, mbali na wahusika bapa, ni lile la wahusika huria au wahusika duara. Hawa huwa na aina mbalimbali za tabia katika riwaya. Hubadilika kitabia, kimawazo,

kinafisia, n.k. Tabia zao hufuatana na mazingira mapya yanayotia nguvu na msukumo mpya, nao hupitia ngazi za kawaida za maisha. Hukua, huumwa na hata kufa panapopasa. Hivyo, huwakilisha uhalisi wa maisha.

Kuikabili hadithi

Katika fani ya riwaya inatubidi kuainisha mambo yafuatayo:

A. Dhamira

- i) **Dhamira kuu** yaweza kupatikana kutokana na huduma za wahusika yaani mhusika na jumuiya yake; mhusika na jinsianavyokabili mazingira katika riwaya; mhusika na itikadi.

Dhamira ndogo ndogo pia huweza kujitokeza katika riwaya.

- ii) **Maudhui** yaani mafunzo, falsafa, n.k. yatokanayo na riwaya nzima.

Maswali ya kujiuliza.

- Je, kichwa cha riwaya kinasadifu maudhui?
- Tumeambiwa nini? Hayo tunayoambiwa yana ukweli wa maisha?
- Sehemu gani imetufurahisha au kutusikitisha zaidi?
- Sehemu gani haitufai au inatufaa?

B. Fani

- i) **Wahusika:** Je, wahusika wanakubalika kwa jamii? Kwa nini? Yupi hakubaliki? Kwa nini? Mhusika gani amependelewa zaidi? n.k.

ii) Mtindo:

- Msanii ametumia lugha namna gani? Je, kuna tamathali za usemi, mafumbo, methali, kejeli, n.k. Picha alizochora msanii zinaeleweka na zimemsaidia kumrahisishia maelezo yake?
- Msanii ametumia mbinu zipi? Mazungumzo, mijadala au hadithi ndani ya hadithi?

C) Muundo

- i) Muundo wa riwaya umeanzaje?
- ii) Msanii anatupelekaje kwenye upeo na tamati?
- iii) Je, msanii amefaulu kujenga kiini kimoja kutokana na mchangamano wa matukio mbalimbali?
- iv) Mandhari yanawiana ama hayawiani na mazingira ya kweli?

D) Kufaulu kwa msanii

Kufaulu au kutofaulu kwa riwaya ya msanii kutategemea jinsi alivyoweza kuonisha maudhui na fani katika kazi yake.

MAZOEZI 1

1. Riwaya ni nini?
2. Lugha inayotumiwa katika riwaya ni ya namna gani?
3. Eleza maana ya mhusika katika hadithi
4. a) Riwaya hujengwa na mambo gani?
b) Eleza sifa na tabia mbalimbali za wahusika.
5. Riwaya huhifadhiwa kwa njia gani ili isisahaulike?
6. Fafanua dhana zifuatazo:
 - a) Mandhari katika riwaya.
 - b) Upeo wa riwaya.
 - c) Mwisho wa riwaya.

2. TAMTHILIA

Huu ni uwanja mpana unaochukua dhana ya sanaa za maonyesho na michezo ya kuigiza. Mara nyingi katika kiwango hiki hushughulikia michezo ya kuigiza zaidi.

Mchezo wa kuigiza hujengwa na wahusika na migogoro iliyomo michezoni. Hiyo migogoro ndiyo inayokuza mwendo wa igizo katika tanzu hii. Migogoro hio, bila shaka huwa na kisa. Kisa na migogoro huendeshwa na wahusika. Wahusika huyawonyesha au kuyapa hayo mazungumzo na vitendo vya kuigiza vinavyotoa sanaa maalumu.

Tamthilia ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili uigizwe jukwaani au usomwe. Lengo kuu ni lile la kutoa maudhui na ujumbe kwa njia ya maigizo.

2.1. Aina za tamthilia

Kuna aina nyingi za tanzu hii. Kuna tamthilia za mapenzi, za kihistoria, za kisiasa, za kidini, n.k. Hizi zote huangukia katika moja ya makundi yafuatayo:

i) Tanzania: ni tamthilia yenye huzuni ndani mwake.

Huweza kuwa na matukio ya vifo na mateso. Mwisho wa tamthilia za aina hii huwa ni wa masikitiko, maanguko na hasara kwa mhusika mkuu au jamii inayoibushwa. Wasomaji au watazamaji hujinasibisha na maangamizi ya mhusika huyo au jamii hiyo.

ii) Ramsa: ni tamthilia zenye kuchekesha kutokana na utani, mzaha, kejeli, matendo yaonyeshayo ujinga, n.k. Uchekeshaji huo hulenga katika kuikosoa jamii, watawala na tabia mbaya na watu binafsi.

iii) Tanzania-Ramsa: tamthilia hizi zina sifa za ramsa lakini ndani ya uchekeshaji wake huwa na tanzia kama vile kuaanguka kwa jamii au maanguko ya mhusika mkuu.

Sanaa hii hukusudiwa kuigizwa jukwaani. Kuna jukwa la akilini kama michezo ya kuigiza ya redioni na jukwaa hasa la hadharani. Mchezo wa kuigiza ili uwe mchezo wa kuigiza sharti uweze kuigizika. Hilo ndilo lengo hasa ya michezo ya kuigiza.

2.2. Mambo ambayo hujenga tamthilia

i) Maudhui: ujumbe na dhamira za mwandishi wa tamthilia, yaani yaliyomo katika tamthilia yake. Mwandishi wa tamthilia kama waandishi wa tanzu nyingine za fasihi, haandiki tu kwa minajili ya kuandika. Ana jambo ambalo anataka kulionyesha jamii. Hivyo, maadili, maonyo, n.k. huweza kupatikana kutoka katika tamthilia.

ii) Fani: tamthilia hujengeka kwa muundo maalumu. Huwa na mwanzo. Mwanzo huu ndio hutujulisha kwa ufupi au pengine kwa mafumbo, yale ambayo tunatazamia kukutana nayo hapo mbele; mwanzo huu husukumwa na mazungumzo ya kitamthilia ambayo yanabeba migogoro ili kitendo kifike kwenye kilele na hatimaye mwisho wa mchezo. Kilele cha tamthilia humfanya mtazamaji apate huruma na hofu; na mwisho huwa na usuluhisho ambao hutuambia hali mpya ilivyo. Matukio, migogoro na mazungumzo huendeshwa na wahusika. Hivyo wahusika ni muhimu sana katika tamthilia.

Tofauti na wahusika wa tanzu zingine, katika tamthilia wahusika hujiweza wenyewe kwa yale wasemayo na watendayo.

Matukio katika tamthilia yana mandhari yake maalumu. Ndiyo maana kila onyesho linafanyika katika mazingira ambayo mwandishi anayachagua.

Kwa kifupi, ili kuwa na tamthilia tunahitaji kuwepo mambo yafuatayo:

- a) **Maudhui:** Mawazo makuu, ujumbe na dhamira za mwandishi.
- b) **Lugha:** mazungumzo ya kitamthilia ambayo ni mazungumzo ya moja kwa moja. Mazungumzo haya licha ya kusukuma kitendo mbele kama tulivyogusia hapo awali, huibusha tabia ya wahusika, wadhifa wao katika jamii, matabaka na matamania yao.
- c) **Muundo:** mwanzo, upeo, mwisho.
- d) **Matukio:** yale yatendekayo katika mchezo.
- e) **Migogoro:** hali ya kutokubaliana mawazo, matendo, n.k. kati ya wahusika. Migogoro hii inaweza kuwa kati ya wahusika binafsi wa kizazi kimoja au kati ya kizazi na kizazi kingine. Pia inaweza kuwa kati ya watawaliwa na watawala, jamii na misukumo ya kijamii au kimazingira iliyomo katika eneo hilo. Hali ya migogoro hufanya mchezo usonge mbele, kwa kitendo cha pili kutokana na kusababishwa na cha kwanza.
- f) **Wahusika:** watu, wanyama, wadudu na viumbe wa kufikirika (majini, mazimwi, n.k.) ambao wanachukua nafasi ya kuiwakilisha jamii katika mchezo. Kuna wahusika wakuu na wadogo.

- g) Mtindo:** tamthilia inaweza kuchukua mtindo wa ishara, yaani huweza kuzungumzia kitu ambacho kinawakilisha kitu kingine. Kwa mfano: Shetani kuwa Mkoloni. Pia tamthilia huweza kuwa katika hali ya uhalisia. Tamthilia nyingine hutumia nyimbo ili kuisisitiza ujumbe.

MAZOEZI 2

1. Tamthilia ni nini?
2. Taja aina za tamthilia kwa kutumia mifano mahususi.
3. Toa tofauti kati ya tanzia na ramsa.
4. Migogoro ina umuhimu gani katika tamthilia?
5. Tamthilia inatofautianaje na Riwaya?

3. USHAIRI

Shairi ni mtungo wa kisanaa, wenye mapigo yenye kufanya mdundo maalumu, na kuwa na miisho yenye sauti tamu zinazofanana. Shairi ni chombo cha kuelezea maisha ya kila siku. Japo kazi za nathari na tamthilia pia hujadili maisha kwa ujumla, lakini shairi la Kiswahili huyasema hayo katika sanaa ya juu ya lugha. Shairi lina usemi ulio mtamu sana kwa maoni yanayopenya yaliyo bora sana.

Watalaamu wengi wa Kiswahili na hususa wale wataalamu wa ushairi wa Kiswahili hukubaliana kuwa ushairi wa Kiswahili ulianza kale kwenye ngoma. Katika nyimbo za mgomani ndiko ushairi wa Kiswahili ulikoanzia na kutoka huko ukaendelea kukua.

Ushairi wa Kiswahili hufunza, huadili, hujadili mazingira, hutoa fikra na busara, hujigamba, husuta, hukejeli, hata kutukana. Heleza mambo ya msiba, ushairi wa Kiswahili hueleza mapenzi, machukivu, maonevu na hisia zote alizo nazo binadamu.

Umbo la ushairi wa Kiswahili, huwa na mizani na vina na hiyo mistari ya shairi. Hayati Mnyampala husema hivi: “Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongezi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa ushairi”.

Shairi hutumia lugha ya picha na huwa na ulinganifu wa vina. Vina hapa, maana yake ni miisho iliyo sawa, silabi za sauti ile ile zilizoko mwisho.

Shairi huwa na ulinganifu wa mizani. Mizani ni idadi sawa ya silabi katika kila msitari, ubeti hadi ubeti. Mizani hiyo inatakiwa kufanana ili kutoa mdundo wa shairi.

Shairi huwa na kituo, yaani mwisho wa ubeti. Maana kamili katika shairi hupatikana wakati shairi hilo linajitosheleza. Mashairi husomwa au huimbwa.

Tuchukue mfano wa ubeti huu:

Jua lililo angani, dunia huangazia.

Nasi tukiwa mwangani, mpaka jua kutua.

Tukabakia gizani, hadi juu kurejea.

Jua tayari ya shairi, hututawala mchana.

Mizani: ni mizani 8 kila nusu mstari kwa hiyo ni mizani 16 kwa mstari.

Vina: kuna kina cha kati, “**ni**” katika kila nusu mstari. Kuna kina cha mwisho, “**a**” katika kila mwisho wa mstari.

Lugha ya shairi ni ya mkato, nyooфу na yenye mvuto na mnato yaani tumbuizi kwa masikio.

Maneno yake ni maneno yaliyoteuliwa ili kukidhi lengo la mshairi.

Ushairi wa Kiswahili hujumuisha **mashairi, tenzi na ngonjera**.

a) Mashairi: Mashairi ya Kiswahili huzungumzia mambo mbalimbali yahusiyo binadamu na mazingira yake. Kuna aina nyingi za mashairi. Yafuatayo ni baadhi tu ya aina ya mashairi:

i) Mashairi ya Simango: haya ni yale mashairi yenye kauli ya simbulio yaaani yenye kumuudhi mtu kwa kumuubua, kumkumbusha wema aliopata kufanyiwa wakati akiwa na dhiki kiasi cha kumwaibisha tu.

ii) Mashairi ya kashifa: yale yenye kutoa siri za mtu, kikundi kidogo cha watu au jamii katika hadhara.

- iii) **Mashairi ya wasifu:** ni mashairi ambayo huelezea sifa z akitu, mtu au jamii. Maelezo yake yanaweza kuwa juu ya tabia au umbile la vitu hivyo.
- iv) **Mashairi ya uzinduzi:** mashairi haya humwamsha mtu kutoka katika hali ya kupumbazwa au kutoelewa mambo. Humfanya mtu apate habari fulani ambayo hakujijua. Hivyo hutanabahisha.
- v) **Mashairi ya waadhi au nyaadhi:** haya hutoa maudhui ya nasaha njema. Yaani maneno ya kumpa mtu ushairi katika njia nyoofu. Pia, mashairi ya kuadibu huingia katika mkumbo huu.
- vi) **Mashairi ya kujigamba:** haya ni mashairi ambayo humwonyesha mshairi akijisifu na kujifaragua. Hujifutua katika shairi lake akaonekana mjuzi wa mambo.
- vii) **Mashairi ya mapenzi:** katika mashairi haya tunaweza kumwona mshairi ambaye penzi linamkera na akikumbuka penzi la zamani lililotiwa doa, n.k.

Lugha ya shairi ni ya mkato, nyoofu na yenye mvuto na mnato yaani tumbuizi kwa masikio. Maneno yake ni maneno yaliyoteuliwa ili kukidhi lengo la mshairi. Shairi hutumia lugha ya picha na huwa na ulinganifu wa vina. Vina hapa, maana yake ni miisho iliyo sawa, silabi za sauti ile ile zilizoko mwisho.

Shairi huwa na ulinganifu wa mizani. Mizani nin idadi sawa ya silabi katika kila msitari, ubeti hadi ubeti. Shairi huwa na kituo, yaani mwisho wa ubeti. Maana kamili katika shairi hupatikana wakati shairi hilo linajitoshereza. Mashairi husomwa au huimbwa.

Ufuatao ni mfano wa beti mbili za shairi la Kiswahili «**Fadhili za Mkulima**» kutoka katika Diwani ya Mnyampala. Shairi hili ni huelezea wasifu wa mkulima.

«Mkulima ni karimu, ni mtu mwenye huruma.

Mkulima ni rahimu, wala hali cha dhuluma.

Mkulima ni tabasamu, hupati kwake hakama.

Fadhili za mkulima, nyingi hazina idadi.

Mkulima mahashumu, wa mahindi na mtama.

Mkulima hukirimu, njaa inapotuuma.

Mkulima ni adhimu, ndiye hutupa uzima.

Fadhili za mkulima, nyingi hazina idadi.»

- b) Utenzi:** utenzi ni sanaa ambayo huelezea tukio maalum. Tukio hilo linaweza kuwa ni la kihistoria katika jamii, la wakati ule ambao jamii inaishi au linalotabiriwa.

Kwa sababu ya uzito wa yale ambayo tenzi huelezea, kwa kawaida tenzi nyingi huanza na dua. Mwandishi humwomba Mola amwongoze katika uandishi wake.

Tukiangalia katika fani, tungo zake huwa ndefu, yaani huwa ni beti nyingi kuliko shairi. Zaweza hata kuzidi mia tatu kufuatana na uzito wa maudhui na ubingwa wa mtunzi. Katika utunzi wa kawaida utungo huhesabiwa kuwa ni utenzi wakati ambapo beti zinavuka ishirini. Utenzi una mizani fupi na mara nyingi ni mizani nane nane katika kila msitari, ingawa kuna nyingine ambazo huwa na mizani nyingi au chache ya hapo.

Mstari wa utenzi huwa na kipande kimoja tofauti na mstari wa shairi ambao umegawanywa katika mistari miwili. Ubeti wa utenzi huwa na mistari minne. Kina cha mwisho katika mstari wowote wa mwisho wa ubeti hakibadiliki.

Zifuatazo ni beti nne za utenzi ambazo zimetolewa kama mfano. Beti hizo zimetoka katika utenzi wa TWAMKUMBUKA KENYATTA uliomo katika MASHAIRI YETU kitabu kilichohaririwa na M.K. Khan.

“Natarabuku na dua

Naombea mwenye Qua

Raisi mwenye murua

Peponi kukaribia

Mola umweke pema

Akae na kuterema

Pasi hofu kumuangama

Wala tabu na udhia.

Twalia tukidadisi
 Tukumbukapo jinsi
 Alivyotenda Raisi
 Siwezi kusimulia

Ninachukua fursa
 Wasomi niwape kisa
 Alivyoanza siasa
 Uhuru kugombania.”

c) Ngonjera: ngonjera ni utunzi wa ushairi ambapo watu wawili huwasiliana au wanaweza kulumbana na kujibizana kishairi.

Katika makala yake, UTUNZI WA USHAIRI WA KISWAHILI, Dr. MASSAMBA D.P.B. anasema,

“... Ngonjera ni aina ya ushairi ambamo twakuta mahojiano na malumbano kati ya watu wa pande mbili. Yaweza kuwa baina ya mtu na mtu au watu na watu. Jambo kubwa kabisa katika ngonjera ni kwamba zenyewe husemwa haziimbwi.”

Naya Mathias Mnyampala ambaye ni bingwa wa utanzu huu katika dibaji ya kitabu chake NGONJERA ZA UKUTA anasema,

“Maana ya ngonjera ni kusoma mashairi, kwa ghibu bila ya kutazama kitabu au karatasi yoyote. Mashairi haya yametungwa ili kujibizana vijana wawili wawili au zaidi. Michezo ya mashairi haya ni lazima yawe na mafunzo ndani yake. Kama hayana mafundisho au vidokezo vya kufurahisha, mchangamsho na kadhalika hayawezi kuitwa ngonjera.

Si laiki ya ngonjera kutumia lugha mbaya ya matusi na mambo ya kipuuzi. Ikiwa mashairi yatakuwa ni ya kipuuzi namna hiyo hayawezi kuitwa ngonjera kamwe.”

Kutokana na maelezo ya wataalam wa hapo juu tunaona wazi kuwa ngonjera, tofauti na mashairi ya kawaida huwa na wahusika ambao hushika nafasi. Mara nyingi huwa na mhusika mwerevu au mjinga. Mwerevu kazi yake humwelimisha mjinga jambo asilojua na hatimaye mjinga hukiri kwamba amepambanukiwa na kuelewa jambo



hilo. Maudhui yake huweza kuwa ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa ujumla.

Utoaji wa ngonjera hutumia sana vitabia. Yaani wahusika hutumia mikono, macho, midomo na viungo vingine vya mwili. Hivyo penye kukonyeza, mhusika hukonyeza ili kusisitiza ujumbe. Hali kadhalika penye mshangao, mhusika huweza kutumbua macho na kuachama mdomo kama ishara ya kupigwa na bumbuwazi, n.k. Uhai wa igizo la ngonjera hutokana na sifa hii ya utumiaji wa vitabia.

Ufuatao ni mfano wa ngonjera ya malumbano kati ya Daktari na Mwalimu kutoka katika MASHAIRI YETU (M.K. Khan-mhariri).

Daktari na Mwalimu

Daktari

Hii kazi ya Mwalimu, kweli haina thamani,
Ni kama mwendawazimu, kelele kutwa shuleni,
Na mimi siheshimu, sitii maanani,
Kazi ya kujivunia, kweli ni ya Daktari.

Mwalimu

Ni wewe mwendawazimu, huna akili kichwani,
Wasema bila fahamu, hujui wasema nini,
Udokta hautimu, bila kufika shuleni,
Kazi njema ya walimu, kutoa watu gizani.

Daktari

Kusoma hailazimu, mtu afike shuleni,
Kuna wengi mumu humu, wasomea barazni,
Na mengi wayafahamu, yaliyomo vitabuni,
Daktari ni muhimu, kwa kuokoa maisha.

Mwalimu

Hilo si maalumu, kuokoa maishani,
Tena unajidhulumu, waingia kufuruni,
Hiyo kazi ya Karimu, ndiye mwenye nusurani,
Kazi njema ya walimu, kutoa watu gizani.

Daktari

Daktari ni muhimu, kukutoa ujingani,
Mtu amekula sumu, maisha ya hatarini,
Budi atajilazimu, afike kwangu nyumbani,
Daktari ni muhimu, kwa kuokoa maisha.

Mwalimu

Asili ya binadamu, yatokana na manani,
Narudi kutakalamu, nililosema mwanzoni,
Asipopenda Karimu, bidiizo zifaeni?
Kazi njema ya walimu, kutoa watu gizani.

Daktari

Hilo nalifahamu, silipingi abadani,
Amri ni ya Karimu, najua toka zamani,
Japo mtu hana damu, asubiri kwa Manani,
Daktari ni muhimu, kwa kuokoa maisha.

Mwalimu

Kidogo natabasamu, na kicheko mdomoni,
Wa tele wendawazimu, moja ni wewe fulani,

Hivyo wale marehemu, hawakwenda ugangani?

Kazi njema ya walimu, kutoa watu gizani.

Daktari

Hilo mimi sikubali, nitafanya nushindani,

Bora kuomba Jalali, si lazima ugangani.

Unapopata ajali, mbona hukai nyumbani?

Daktari ni muhimu, kwa kuokoa maisha.

Mwalimu

Hayo yako sikubali, na wala siyaamini,

Tokea enzi azali, hako Daktari nchini,

Watu hupata thakili, hutibiwa majumbani,

Kazi njema ya walimu, kutoa watu gizani.

...../.....

MAZOEZI 3

1. Kuna tofauti gani kati ya mashairi na tenzi?
2. Lugha ya shairi ni lugha ya namna gani?
3. Matumizi ya vitabia katika ngonjera husaidia nini?
4. Je, katika jamii ya Wanyarwanda kuna kuna utungo wa ngonjera?
5. Utungo wa utenzi huwa mrefu kwa sababu gani?

SURA YA TATU: NGELI ZA MAJINA

Ngeli ni nini?

Ngeli ni utaratibu wa taluuma ya sarufi ya lugha katika kupanga aina za majina. **Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004)**, inaeleza ngeli kama kundi la nomino katika baadhi ya lugha lenye sifa zinazofanana. Ngeli za Kiswahili zaweza kuanishwa kwenye makundi mbalimbali. Tutaanza kuzijadili ngeli hizo moja moja ili tujue ni mambo yapi yanayozihusu. Katika Kiswahili, jina ni neno linalotambulisha mtu, kitu ama jambo. Majina haya ya Kiswahili yanaweza kugawika katika makundi mbalimbali kulingana na upatanisho wa kisarufi wa maneno hayo, yaani viambishi vyake vya awali. Mgawo huo huitwa ngeli. Ngeli ni utaratibu wa sarufi katika lugha ambapo majina ya aina moja, kulingana na viambishi awali, hupangwa pamoja.

Katika Kiswahili tunazo ngeli nane.

NGELI YA KWANZA: A-WA

Ngeli hii hujumuisha majina yote ya vitu vyenye uhai isipokua mimea. Hivyo majina yote ya watu, wanyama, ndege, wadudu yamo katika kundi hili.

Pia majina ya Mungu, mashetani, malaika katika ngeli hii kiambishi ni **A-** katika umoja na **WA-** katika wingi.

MATUMIZI YA NGELI YA A-WA

Umoja

Mtoto analia

Nguruwe anachinjwa

Malaika amemshukia

Nyoka anatambaa

Wingi

Watoto wanalia

Nguruwe wanachinjwa

Malaika wamemshukia

Nyoka wanatambaa

VIVUMISHI VYA NGELI YA A-WA**A. Vivumishi vya kuonyesha****Umoja**

Mtu huyu

Mtu huwo

Mtu yule

Wingi

Watu hawa

Watu hao

Watu wale

B. Vivumishi vya kumilikisha**Umoja**

Punda wako amepotea

Mzee wangu amenisumbua

Nywele zake ni fupi sana

Wingi

Punda wenu wamepotea

Wazee wetu wametusumbua

Nywele zao ni fupi sana

Tanbihi: Iangaliwe kwamba katika kumilikisha kuna majina ya ngeli ya A-WA ambayo hayafuati mkondo huu. Mengi ya majina hayo ni yale yanayoonyesha uhusiano wa watu.

Kwa mfano hatusemi:

Baba wangu

Mama wangu

Bali tunasema:

Umoja

Baba yangu

Mama yako

Ndugu yake

Rafiki yetu

Shangazi yao

Wingi

Baba zetu

Mama zenu

Ndugu zao

Rafiki zetu

Shangazi zao

Majina hayo ni kama: kaka, dada, wifi, shangazi, mjomba, shemeji, binamu, n.k.

C. Vivumishi vya kuuliza.

Mwanajeshi yupi amekufa?

Wanajeshi wapi wamekufa?

Msichana gani ameolewa?

Wasichana gani wameolewa?

D. Vivumishi vya idadi

Mwalimu mmoja

Walimu wawili

Watatu

Wanne

Watano

Sita

Saba

Wanane

Tisa

E. Vivumishi vya kurejesha

Mimi mwenyewe nilifanya jaribio

Wewe mwenyewe ulifanya kazi ya nyumbani

Yeye mwenyewe alifukuzwa kazini

Kuku mwenyewe amekula mahindi

Sungura mwenyewe alimdanganya Fisi

F. Vivumishi vya sifa

Mtoto mpole amekufa → watoto wapole wamekufa

Msichana mwema anafurahi → Wasichana wema wanafurahi

Mpishi mzuri anakuja → Wapishi wazuri wanakuja

Mwanafunzi mnene anafaulu → Wanafunzi wanene wanafaulu

Msichana mwembamba hupendwa → Wasichana wembamba hupendwa

MAZOEZI 1

1. Badilisha sentensi zifuatazo katika wingi.
 - a) Mkulima huyu analima vizuri.
 - b) Mtoto wake hana maringo.
 - c) Mwanamke huyu ni mnene.
 - d) Mbwa wake ni mkali.
 - e) Daktari wake amefika.
2. Sahihisha sentensi zifuatazo.
 - a) Mtu huyu inakwenda wapi?
 - b) Mbwa yake ilikufa jana.
 - c) Dereva hii ana wazimu.
 - d) Ambia watoto ile waje hapa.
 - e) Kijana kile kinatembea vizuri.
 - f) Nyuki zilipoingia nyumbani, zilikula watu yote.
 - g) Mwizi ule umekimbia.
 - h) Punda inakimbia.
 - i) Nyani hii ni kubwa sana.



NGELI YA PILI: U-I

Ngeli hii huchukua majina yote ambayo kwenye kitenzi huwa na kiambishi ngeli **U-** katika umoja na **I-** katika wingi.

Majina ya ngeli hii mengi yanatokana na majina ya miti (mchungwa, mwembe, mgomba, mpapai, mnazi, mnanasi, n.k.), baadhi ya viungo vya mwili (mdomo, mguu, mkono, msuli, mshipa, mgongo, n.k.), vyombo na mengineyo.

MATUMIZI YA NGELI HII

Umoja

Mti umeanguka

Mkono umevunjika

Mlango umeharibika

Mto unafurika

Wingi

Miti imeanguka

Mikono imevunjika

Milango imeharibika

Mito inafurika

A. Vivumishi vya kuonyesha

Mlango huu unaharibika

Mlango huo unaharibika

Mlango ule unaharibika

Milango hii inaharibika

Milango hio inaharibika

Michungwa ile inapendeza

B. Vivumishi vya kumiliki

Mgomba wangu uliungua

Migomba yangu iliungua

Mpera wako ulikatwa

Mipera yenu ilikatwa

Mgomba wake ulizaa ndizi

Migomba yao ilizaa ndizi

C. Vivumishi vya kurejesha

Msitu wenyewe unaoungua ni ule

Misitu yenyewe iliyoungua ni ile

Mlango wenyewe uliofunguliwa ni ule

Milango yenyewe iliyofunguliwa ni ile

Mto wenyewe uliofurika ni ule

Mito yenyewe iliyofurika ni ile

D. Vivumishi vya idadi

Msumari mmoja umepotea

Misumari miwili imepinda

Misumari mitatu

Misumari minne

Misumari mitano

Misumari Øsita

Misumari Øsaba

Misumari minane

Misumari Øtisa

Misumari mingi

Misumari michache



E. Vivumishi vya kuuliza

Umoja

Ni mlango upi umefungwa?

Ni mlango gani umeupenda?

Mguu upi umejeruhiwa?

Wingi

Ni milango ipi imefungwa?

Ni milango gani umeipenda?

Miguu ipi imejeruhiwa?

F. Vivumishi vya sifa.

Ni mti mrefu sana → mirefu sana

Ni mti mkubwa sana → mikubwa sana

Ni mti mfupi sana → mifupi sana

MAZOEZI 2

1. Weka katika umoja au wingi majina yafuatayo.

Umoja	Wingi
a)	Miguu
b) Mkono
c) Mswaki
d)	Mipira
e)	Mishumaa
f) Mchuzi
g)	Mikebe
h)	Wafagiaji

2. Chagua neno linalofaa na uliandike katika nafasi zilizoachwa wazi.

a) Alipanda mti (mmoja, mingi, nyingi)

- b) Mkeka Mama (ya, wa, ka)
- c) Mpapai huzaa mapapai mengi (huyu, hii, huo)
- d) Miguu imepinda (ile, iyo, yile)
- e) Sitaki kukusaidia kubeba mtungi (ule, ile, yule)

NGELI YA TATU: KI-VI

Ngeli hii huchukua majina ya vitu, vyombo au viungo mbalimbali vya mwili. Ngeli hii katika umoja ni **KI-** na wingi ni **VI-**.

Mifano:

Kisu →visu

Kikapu →vikapu

Kiumo →viuno

Kichwa →**vichwa**

Kisigino →visigino

Kikombe →vikombe

Kitabu →vitabu

Kioo →vioo

Chumba →vyumba

MATUMIZI YA NGELI HII

Kikombe kimevunjika

Vikombe vimevunjika

Kisu kimepotea

Visu vimepotea

VIVUMISHI VYA NGELI HII**A. Vivumishi vya kuonyesha**

Kikapu hiki kinapendeza →Vikapu hivi vinapendeza

Kikapu hicho kinapendeza →Vikapu hivyo vinapendeza

Kitabu kile kinafurahisha →Vitabu vile vinafurahisha

B. Vivumishi vya kumiliki

Kikapu changu ni kirefu →Vikapu vyetu ni virefu

Kikapu chako ni kirefu →Vikapu vyao ni virefu

Kiberiti chake kimekwisha →Vibereti vyake vimekwisha

Kibereti chao kimekwisha →Vibereti vimekwisha

C. Vivumishi vya kurejesha

Choo chenyewe kinanuka →Vyoo vyenyewe vinanuka

Chungu chenyewe kinavunjika →Vyungu vyenyewe vimevunjika

Kisu chenyewe kinanikata →Visu vyenyewe vinanikata

D. Vivumishi vya kuuliza

Kibereti kipi kimepotea? →Vibereti vipi vimepotea?

Kibereti gani kimepotea? →Vibereti gani vimepotea?

Kisu gani ni kizuri? →Visu gani ni vizuri?

Kisu kipi ni kizuri? →Visu vipi ni vizuri?

E. Vivumishi vya idadi**Umoja**

Kikombe kimoja kimeimbwa

Wingi

Vikombe viwili vimeibwa

Vitatu

Vinne
 Vitano
 Sita
 Saba
 Kumi
 Vingi
 Vichache

F. Vivumishi vya sifa

Kitabu kizuri kimepotea → Vitabu vizuri vimepotea

Kilima kirefu kinapendeza → Vilima virefu vinapendeza

Kitambaa kikubwa kimefuliwa → Vitambaa vikubwa vimefuliwa

MAZOEZI 3

1. Badilisha majina yafuatayo katika wingi au umoja.

Umoja	Wingi
a) Kibiriti
b) Kioo
c)	Vyandarua
d) Cheo
e) Kiwanja
f) Kiboko
g)	Visiwa

2. Badilisha sentensi zifuatazo katika wingi

- Kitambaa kipya hiki kinavutia.
- Kiko chake kiko mezani.

- c) Sitaki kununua kitu chochote.
 - d) Chandarua kile kikubwa kinafaa kufunikia kitanda.
 - e) Chombo chote kimejaa viazi.
 - f) Kisu kikali hiki kinafaa kukatia kipande cha nyama.
 - g) Kikombe ambacho kinavuja kimezibwa
 - h) Kitanda chenyewe hiki ni kibaya.
 - i) Chochote kile kinafaa kwa kazi hii.
3. Chagua neno linalofaa na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.
- a) Kikombe hiki ni (yangu, changu, lake)
 - b) ni chumba chao (ile, hii, lile, kile)
 - c) Cheo kinamzuzua (yake, chake, wake)
 - d) Jana tulinunua viberiti (mingi, mengi, nyingi, vingi)
 - e) Kiazi kimeliwa (lote, yote, vyote, chote)
4. Sahihisha sentensi zifuatazo:
- a) Chungu iliyovunjika ni yetu.
 - b) Chuma zile zipelekwe pale.
 - c) Chumba yao ya kulia ni chafu.
 - d) Chakula yote imeharibika.
 - e) Mtoto yake alivunja kikombe yao.
 - f) kisu yao ilipotea kesho.
 - g) Kibuyu ambayo imenunuliwa imeibiwa.
 - h) Nipe kijiko yangu.
 - i) Wapi unapeleka kiko hilo?

5. Andika majina ishirini yaliyo katika ngeli ya tatu.

NGELI YA NNE: LI-YA

Maneno yanayoingia katika ngeli hii huwa na umoja na wingi. Hata hivyo wingi wa majina ya ngeli hii hupatikana kwa kupachika kiambishi awali **ma-** kwenye jina ambalo limo katika umoja.

Baadhi ya majina yanayoingia katika ngeli hii:

Jibu – majibu	kabati – makabati
Jeshi – majeshi	bega – mabega
Jeneza – majeneza	gurudumu – magurudumu
Jambazi – majambazi	gari – magari
Jingo – majengo	dirisha – madirisha
Jinni – majini	koti – makoti
Jaribio – majaribio	shamba – mashamba
Jiwe – mawe	shati – mashati
Jicho – macho	pera – mapera
Jambo – mambo	jino – meno

MATUMIZI YA NGELI HII

Umoja

Jahazi limezama baharini
Jibu limepatikana
Jambazi lilikamatwa jana

Wingi

Majahazi yamezama baharini
Majibu yamepatikana
Majambazi yalikamatwa jana

VIVUMISHI VYA NGELI HII**A. Vivumishi vya kuonyesha**

Ganda hili linateleza →Maganda haya yanateleza

Gari hilo lilivunjika →Magari hayao yalivunjika

Ganda lile linateleza →Maganda yale yanateleza

B. Vivumishi vya kurejesha

Shamba lenyewe linalimwa →Mashamba yenyewe yamelimwa

Bega lenyewe limevunjika →Mabega yenyewe yamevunjika

Jambazi lenyewe linashikwa →Majambazi yenyewe yanashikwa

C. Vivumishi vya kumiliki

Koti langu limeibwa →Makoti yangu yameibwa

Koti lako limeibwa →Makoti yenu yameibwa

Koti lake limeibwa →Makoti yao yameibwa

D. Vivumishi vya kuuliza

Jiwe lipi limerushwa? →Mawe yapi yamerushwa?

Jiwe gani limerushwa? →Mawe gani yamerushwa?

Juma lipi tutapumzika? →Majuma yapi tutapumzika?

Juma gani tutapumzika? →Majuma gani tutpumzika?

E. Vivumishi vya idadi**Umoja**

Shamba moja lililimwa

Wingi

Mashamba mawili yalilimwa

matatu
manne
sita
saba
machache
mengi

F. Vivumishi vya sifa

Koti kubwa limeletwa → Makoti makubwa yameletwa

Jingo refu limeanguka → Majengo marefu yameanguka

Kabati zuri limevunjwa → Makabati mazuri yamevunjwa

MAZOEZI 4

1. Badilisha katika wingi tungo hizi.
 - a) Chungwa lile halijaoza.
 - b) Mimi sitaki jembe lile.
 - c) Ulinunua jumba kubwa.
 - d) Jino lake linauma vibaya.
 - e) Shamba ambalo limelimwa litapandwa.
 - f) Gunia lile limetoboka.
 - g) Goti ambalo lilijeruhiwa limepona.
 - h) Jina ambalo liliandikwa limefutwa.
 - i) Shauri hili halikukubaliwa na wakubwa.

2. Tungo zifuatazo zina makosa.

- a) Maziwa hii iko na uchafu.
- b) Alinipiga na jiwe ile.
- c) Sitaki kununua machungwa ile na mapera hii.
- d) Gari hili imebeba watu mingi sana.
- e) Yeye iko karibu na jengo ile.
- f) Yai anayotaka kununua ni kubwa.
- g) Goti ambayo yana vidonda imefungwa vitambaa.
- h) Shoka inatiwa mpini mpya.
- i) Duka yenyewe imejaa bidhaa.
- J) Shamba yenye miti mingi imeuzwa.

NGELI YA TANO: U-

Ngeli hii inatumika kwa majina ambayo hayawezi kuwekwa katika wingi, na ni majina yenye kuonyesha vitu ambavyo havishikiki. Yaani inachukua majina ya dhahania (maarifa). Kiambishi ngeli katika kitenzi ni **u-** katika umoja (na wingi). Baadhi ya majina ambayo yamo katika katika ngeli hii ni haya yafuatayo: ulafi, uchoyo, ufupi, ukubwa, udogo, urembo, weusi, wembamba, ujanja, ujuzi, uzee, umaskini, ulevi, ulozi, uvivu, utajiri, uchovu, utakatifu, uovu, udhaifu, n.k.

MATUMIZI YA NGELI HII

Umoja

Ujinga ulimfanyisha makosa

Utajiri unamzidi

Weusi unampendeleza

Wingi

Ujinga uliwafanyisha makosa

Utajiri unawazidi

Weusi unawapedeza

VIVUMISHI VYA NGELI HII

A. Vivumishi vya kuonyesha

Unene huu ni mbaya

Unene huo ni mbaya

Ufupi ule unashangaza

B. Vivumishi vya kumiliki

Weusi wangu unapendeza → Weusi wetu unapendeza

Ujanja wako unazidi → Ujanja wenu unazidi

Uvivu wake haupendezi → Uvivu wao haupendezi

C. Vivumishi vya kurejesha

Uzuri wenyewe unampendeza → Uzuri wenyewe unawapendeza

Ujuzi wenyewe unamshinda kabisa → Ujuzi wenyewe unawashinda kabisa

Utakatifu wenyewe ni wa kulazimishwa

D. Vivumishi vya kuuliza

Urafiki gani unakuchukiza? → Urafiki upi unawachukiza?

Ukarimu gani unaouzungumzia? → Ukarimu gani mnaouzungumzia?

Ni ujanja upi alitumia? → Ni ujanja gani walitumia?

Ujinga upi unazidi?

E. Vivumishi vya idadi

Katika ngeli hii, huwezi kupata vivumishi vya idadi kwa sababu majina ya maarifa haya hesabiki.

F. Vivumishi vya sifa

Utajiri mkubwa unakufanya ujivune → Utajiri mkubwa unawafanya mjivune

Ujuzi mdogo ulisababisha kushindwa

Urembo mkubwa si mzuri

NGELI YA SITA: U-I-ZI

Majina yaliyomo katika ngeli hii hutambulishwa kwa viambishi ngeli **u-** na **i-** katika umoja na kiambishi **zi-** katika wingi.

Yafuatayo ni baadhi ya maneno ambayo yamo katika ngeli hii:

Ukuta – kuta, ubao – mbao, barabara, njia, alama, sauti, nyumba, nguo, suruali, ufunguo – funguo, uso – nyuso, ulimi – ndimi, akili, baisikeli, kalamu, karatasi, ndege, ukucha – kucha, ufagio – fagio, ufito – fito, wayo – nyayo, wimbo – nyimbo, n.k.

MATUMIZI YA NGELI HII**Umoja**

Barabara imenyooka

Sauti imemkauka

Baisikeli imeibwa

Kalamu inaandika

Ndege inatua Kanombe

Ukuta umebomoka

Wimbo unafurahisha

Ukucha umeng'oka

Ufunguo umepotea

Unyasi umekauka

Wingi

Barabara zimenyooka

Sauti zimewakauka

Baisikeli zimeibwa

Kalamu zinaandika

Ndege zinatua Kanombe

Kuta zimebomoka

Nyimbo zinafurahisha

Kucha zimeng'oka

Funguo zimepotea

Nyasi zimekauka

VIVUMISHI VYA NGELI HII

A. Vivumishi vya kuonyeha

Karatasi hii imechanika →Karatasi hizi zimechanika

Karatasi hiyo imechanika →Karatasi hizo zimechanika

Karatasi ile imechanika →Karatasi zile zimechanika

Wavu huu umekatika →Nyavu hizi zimekatika

Wavu huo umekatika →Nyavu hizo zimekatika

Wavu ule umekatika →Nyavu zile zimekatika

B. Vivumishi vya kumiliki (sha)

Ndege yangu imeanguka →Ndege zetu zimeanguka

Ulimi wangu umeumia →Ndimi zetu zimeumia

Ulimi wako umeumia →Ndimi zenu zimeumia

Ulimi wake umeumia →Ndimi zao zimeumia

C. Vivumishi vya kurejesha

Akili yenyewe imevurugika →Akili zenyewe zimevurugika

Suruali yenyewe imechafuka →Suruali zenyewe zimechafuka

Baiskeli yenyewe imeibwa →Baiskeli zenyewe zimeibwa

Uzi wenyewe umekatika →Nyuzi zenyewe zimekatika

Ubao wenyewe umefutwa →Mbao zenyewe zimefutwa

Ufunguo wenyewe umepotea →Funguo zenyewe zimepotea

D. Vivumishi vya kuuliza

Suruali ipi inakubana? → Suruali zipi zinakubana?

Karatasi ipi/gani imechanika? → Karatasi zipi/gani zimechanika?

Wimbo upi umekufurahisha? → Nyimbo zipi zimekufurahisha?

Uso upi unakupendeza? → Nyuso zipi zinakupendeza?

Ukucha upi/gani umerefuka? → Kucha zipi/gani zimerefuka?

E. Vivumishi vya idadi

Ndege moja imepotea

Wembe moja umeibwa

Ndege mbili zimepotea

Nyembe mbili zimeibwa

Ndege tatu zimepotea

Nyembe tatu zimeibwa

Ndege tano zimepotea

Nyembe nne zimeibwa

Ndege nyingi zimepotea

Nyembe tano zimeibwa

Ndege chache zimepotea

Nyembe nyingi zimeibwa

F. Vivumishi vya sifa

Nyumba nzuri imejengwa → Nyumba nzuri zimejengwa

Kalamu ndefu inaandika → Kalamu ndefu zinaandika

Baiskeli mpya inauzwa → Baiskeli mpya zinauzwa

Karata nyepesi imechanika → Karata nyepesi zimechanika

Ufa mkubwa umezibwa → Nyufa kubwa zimezibwa

Ufagio mrefu umepotea → Fagio ndefu zimepotea

Ubao mweusi umefutwa → Mbao nyeusi zimefutwa

MAZOEZI 5

1. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia viambishi ngeli vinavyofaa.

- a) Barua hizitufikia jana asubuhi.
- b) Nguo yakemeraruka.
- c) Bahasha walizonunua sizuri.
- d) Meza zetumevunjika.
- e) Ndizi tulizonunuameiva.
- f) Njia hizo ha.....pitiki wakati wa masika.
- g) Nyimbo ha.....jasikilizwa.
- h) Nyumba ilelijengwa mwaka uliopita.
- i) Karai ya maji ha.....javuja hata kidogo.

2. Badilisha sentensi zifuatazo katika umoja.

- a) Ndimi zilizokuwa na vidonda zimetibiwa.
- b) Karai zilizotoboka zimezibwa.
- c) Nyavu ambazo zimechanika hazijatengenezwa.
- d) Kamba ambazo hutengenezwa ni ngumu.
- e) Tambi ambazo amenunua ni nyeupe.
- f) Nyakati hizi sizakucheza.
- g) Kwa nini hutaki kuniletea sabuni zangu?
- h) Ajali ilitokea, wasafiri wengi waliharibika nyuso.
- i) Nguo zilizoanikwa hazijakauka.
- j) Nyama hizi haziwezi kuliwa na vibogoyo.
- k) Ndimi nyekundu.

- l) Nyundo zake.
- m) Ndege zote.
- n) Shida hizi.
- o) Kazi ni ngumu.
- p) Nyufa zile ni pana.

3. Sentensi zifuatazo zina makosa, zisahihishe.

- a) Kuta hii zina nyufa mingi sana.
- b) Nenda pale upewe panga moja.
- c) Nywele yake kwisha kuwa mrefu.
- d) Ukucha ule umeng'olewa.
- e) Ndevu kake hunyolewa kila siku.
- f) Mwambiye kuwa mtakuja pande hii.
- g) Uji ambayo tulipewa ulikuwa mtamu.
- h) Taa ambalo tunawasha usiku halioni vizuri.
- i) Karatasi ambako tumenunua ni kazuri.
- j) Ua ambaye atachanua atakatwa.

4. Andika majina thelathini yaliyomo katika ngeli hii.

NGELI YA SABA: PA-M-KU

Ngeli hii huchukua huchukua majina yote ya mahali na viambishi vyake katika vitenzi huwa na viambishi nafsi viambata **pa-**, **m-** au **ku-**. Kwa kawaida katika ngeli hii mahali panapozungumziwa panaweza kujulikana kwa ujumla tu (**ku-**), waziwazi (**pa-**) au pakawa ndani ya kitu (**m-**).

MATUMIZI YA NGELI HII

Hospitalini kuna mawe

Ofisini mna nyoka

Sokoni kuna wauzaji

Darasani mna wanafunzi

Kigali pana/kuna magari mengi

Kichwani kwangu kuna chawa

Kichwani pangu pana chawa

Tanbihi: Kama unasimulia juu ya mahali, nje, waziwazi (ujumla wa mahali) unatumia **pa-** au **ku-**.

VIVUMISHI VYA NGELI HII**A. Vivumishi vya kuonyesha****Pa-**

Mahali hapa pana maji

Mahali hapo pana maji

Mahali pale pana maji

Shuleni hapa pana wanafunzi hodari

Kibuye hapo pana miamba

Ziwani pale pana miamba

M-

Bwenini humu mna harufu mbaya kabisa

Darasani humo mna wanafunzi wengi

Darsani mle mna wanafunzi wengi

Ku-

Chuoni huku kuna walimu wa kutosha

Kigali huko kuna watu wabaya kweli

Msituni huku kuna Simba mkali

Msituni huko kuna Simba mkali

B. Vivumishi vya kumiliki (sha)**Pa-**

Gisenyi pangu panapendeza →Gisenyi petu panapendeza

Mahali pako panapendeza →Mahali penu panapendeza

Mahali pake panapendeza →Mahali pao panapendeza

M-

Chumbani mwangu mna wageni → Chumbani mwetu mna wageni

Nyumbani mwako mna giza →Nyumbani mwenu mna giza

Nyumbani mwake mna giza → Nyumbani mwao mna giza

Ku-

Kazini kwangu kunavutia watu →Kazini kwetu kunavutia watu

Nyumbani kwako kunapendeza watoto →Nyumbani kwenu kunapendeza watoto

Njiani kwake kuna matope →Njiani kwao kuna matope

Butare kao kuna matatizo

C. Vivumishi vya kurejesha**Pa-**

Kabaya penyewe pana milima mingi

Duniani penyewe pana dhambi za kuhangaikisha Mungu

M-

Mtoni mwenyewe mna mamba

Darasani mwenyewe mna watoto

Ndani mwenyewe mna mtama

Kanisani mwenyewe mna Wakristo

Ku-

Nje kwenyewe kuna baridi

Hewani kwenyewe kuna dalili za mvua

Shuleni kwenyewe kuna mchezo wa mpira

D. Vivumishi vya kuuliza

Pa-

Mahali papi panapendeza?

Mahali gani panapendeza?

Ku-

Mahali kupi kuna waimbaji?

Sokoni kupi kuna ndizi?

Shuleni gani kuna vitabu?

M-

Darasani mpi mna wanafunzi?

Chumbani mpi mna kuku?

Chumbani gani mna kuku?

E. Vivumishi vya idadi

Mahali pamoja pana matope

Mahali pawili pana matope

Mahali tisa pana matope

Mahali tisa pana matope

F. Vivumishi vya sifa

Nje pazuri ni hapa

Mahali pabaya/pachafu kunachukiza

Shuleni kusafi kunapendeza

Shuleni kuchafu kunanuka mbaya

Darasani msafi kunapendeza

MAZOEZI 6

1. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia viambishi ngeli vinavyofaa.
 - a) Machungwa ni matundatamu.
 - b) Mbuzi yule nieusi.
 - c) Kazi yake nibaya sana.
 - d) Kijana yule amevaa kiatueusi.
 - e) Kifaruingine kuja mbio.
 - f) Kibokole ...na fundo nyingi.
 - g) Ugonjwa wake ha.....tapon.
 - h) Ninataka chandaruaekundu.
 - i) Kitambaa hiki nizuri sana.

- j)kubwa yule anataka kazi.
- k) Mikaritusi ni mitirefu mno.
- l) Mahaliakemechafuka sana.
- m) Ni vipande ...ngapi unataka?
- n) Vitabu hivi ni ...kuukuu sipya.
- o) Kiroboto ...meingia mguuniake.
- p) Cheti hikikina mhuri.
- r) Shangaziliibiwa vifaaake.
- s) Baba alitujengea nyumbazuri.
- t) Alimtukana rafikike.
- u) Ndugu atakayekuja nidogo wake.

NGELI YA NANE: KU-

Ngeli hii inatumika sawa katika umoja na wingi. Katika umoja kiambishi ni **ku-** na wingi tena ni **ku-**. Maneno yamo katika ngeli hii ni baadhi ya vitenzi ambavyo vinaitwa **vitenzi-jina**.

MATUMIZI YA NGELI HII

Kucheka kunampendeza → Kucheka kunawapendeza

Kuvaa kunamchelewesha → Kuvaa kunawachelewesha

Kujifunza kulimletea faida → Kujifunza kuliwaletea faida

Kusali bila ujanja kutamfikisha mbinguni → Kusali bila ujanja kutawafikisha mbinguni

VIVUMISHI VYA NGELI HII

A. Vivumishi vya kuonyesha

Kuimba huku kunamfurahisha

Kuimba huku kunawachokesha

Kucheza kule kunampendeza

Kunywa kule kunamzidi

B. Vivumishi vya kuuliza

Ni kulala kupi/gani kunampendeza?

Ni kula kupi/gani kunawafurahisha?

Kuvaa gani kuanipendeza?

Kuvaa kupi kuanipendeza?

C. Vivumishi vya kumiliki (sha)

Kujilinda kwangu kuliniokoa

Kulala kwak kunamletea uvivu

Kuvaa kwao hakupendezi

D. Vivumisha vya kurejesha

Kusemasema kwenyewe kulimletea matatizo

Kuiba kwenyewe kulimletea kifo

Kufanya mapenzi kwenyewe kulimletea UKIMWI (SIDA)

Kubaka kwenyewe kulimsababisha kufungwa

E. Vivumishi vya sifa

Kula kubaya kunasumbua watoto

Kulima kuzuri kunaleta mazao ya kutosha

Kunywa kubaya kunasababisha matatizo

MAZOEZI 7

1. Tumia vitenzi jina vifuatavyo katika kutunga sentensi.

Kuchoka, kufuta, kula, kushiba, kuiba, kusafiri, kupigana, kuchora, kupiga.

2. Andika vitenzi jina vifuatavyo katika hali ya kanushi.

Kukauka, kuadhibu, kunywa, kufa, kulima, kupiga, kula, kuacha, kufufuka, kuisitiza.

3. Tumia kiambishi kiwakilishi (-ko-) katika vitenzi vya sentensi zifuatazo:

- a) Kucheza kwa mpira ambako tunaenda uwanjani kunavutia watazamaji.
- b) Kuchelewa ambako mwanafunzi huyu anafanya, kunarudisha maendeleo yake nyuma.
- c) Kusoma ambako anafanya kila siku kutamletea matunda mazuri.
- d) Kulima ambako kunafanywa katika shamba hili kutakuza mimea upesi.
- e) Kukimbia ambako anafanya ni hatari kwake.

SURA YA NNE: USEMI HALISI NA USEMI WA TAARIFA

Usemi halisi ni nini?

Usemi halisi ni yale maneno yanayotamkwa na mtu yakiwa katika hali yake ya kwanza.

Usemi wa taarifa ni nini?

Iwapo mtu anataka kuwaambia wengine maneno ambayo yalizungumzwa na mtu mwingine bila ya kupotosha, kupunguza au kuongeza maana ya jambo analotaka kulitolea maelezo, basi maneno hayo anayosema huitwa **usemi wa taarifa**.

Katika usemi wa taarifa kuna mambo muhimu ya kuzingatiwa ili usemi huo wa taarifa uwe sahihi.

1. Nafsi ya kwanza hubadilika na kuwa katika nafsi ya tatu.

Mifano:

Mimi hugeuka **yeye**

Sisi hugeuka **wao**

2. Badala ya kutumika wakati uliopo **-na-**, wakati uliopita **-li-** ndio hutumika.

Kwa mfano.

Nina kazi nyingi ofisini. (Hugeuka)

→Alisema kwamba alikuwa na kazi nyingi ofisini.

3. Alama za kufunga na kufungua maneno ("") hazitumiki katika usemi wa taarifa.
4. Alama za kuuliza (?) na za kushangaa (!) hazitumiki kwenye usemi wa taarifa.
5. Katika kuandika usemi wa taarifa mahali penye wakati ujao **-ta-** kwenye usemi halisi hugeuka na kuwa **-nge-**.

6. Baadhi ya maneno hubadilisha umbo yanapotumika katika msemo wa taarifa.

Kwa mfano.

- **hapa** huwa **hapo**
- **leo jioni** huwa **siku hiyo jioni**
- **wakati huu** hugeuka **wakati huo**
- **watu hawa** huwa **watu hao**
- **kwetu** hugeuka **kwao**
- **kwangu** hugeuka **kwake**
- **sasa** huwa **wakati huo**

7. Mojawapo ya maneno yafuatayo hutumika katika usemi wa taarifa: **kuwa, kama, kwamba.**

Mifano ya usemi halisi na usemi wa taarifa

Ifuatayo ni misemo ya asili na mifano yake katika misemo ya taarifa.

- a) “ Utanikuta mjini jioni hii”. Juma alimweleza rafiki yake.
→ Juma alimweleza rafiki yake kuwa angemkuta mjini jioni ile.
- b) “Wanangu dunia ya leo inawapasa mfanye kazi kwa bidii”. Mzee aliwaambia watoto wake.
→ Mzee aliwaambia watoto wake kuwa katika dunia ya siku hizi iliwapasa wafanye kazi kwa bidii.
- c) “Mnataka kununua nini hapa dukani?” Mama aliwauliza watoto wake.
→ Mama aliwauliza watoto wake kitu ambacho walitaka kununua dukani pale.
- d) “Inaelekea mvua itakayonyesha usiku huu itakuwa kubwa sana”. Mzee alisema.
→ Mzee alisema kwamba ilielekea kuwa mvua ambayo ingenyesha usiku ule ingekuwa kubwa.



- e) “Nitakapokuwa mtu mzima nitajijengea nyumba kubwa na nzuri”. Motto aliwaambia wenzake.
- Mtoto aliwaambia wenzake kuwa angejijengea nyumba kubwa na nzuri wakati ambapo angekuwa mtu mzima.
- f) “Saa za jioni tutakutana kuandaa mipango ya sherehe za kuadhimisha miaka kumi na nane ya uhuru na safari hii ni lazima iwe mizuri”. Akasema mkuu wa mkoa.
- Mkuu wa mkoa alisikika akasema kuwa wangekutana naye saa za jioni ili wapange mipango ya kuadhimisha miaka kumi na nane ya uhuru na alizidi kusema kuwa safari hiyo ilikuwa lazima mipango hiyo iwe mizuri.
- g) “Ni vibaya kwa wanafunzi kuvuta sigara kwa sababu sigara huharibu afya, humaliza pesa na huweza kusababisha vita”. Mwalimu mkuu aliwaeleza wanafunzi wake.
- Mwalimu mkuu aliwaeleza wanafunzi wake kwamba ilikuwa vibaya kwaokuvuta sigara kwani sigara ingeweza kuharibu afya, pesa na pia ingeweza kusababisha vita.
- h) “Kuanzia wakati huu mimi mwenyewe ninaanza kuamrisha majeshi yote kwa sababu viongozi niliowaweka wameshindwa wajibu wao”. Alisikika Amiri Jeshi Mkuu akisema.
- Amiri Jeshi Mkuu alisikika akisema kuwa angeanza hapo hapo kuamrisha majeshi yote yeye mwenyewe kwa sababu viongozi aliokuwa amewaweka walishindwa wajibu wao.

SURA YA TANO: UTUNGAJI

1. INSHA

Insha ni mtungo wa maneno kwa mtindo wa nathari juu ya jambo fulani. Insha ni maelezo ya mawazo au habari kuhusu jambo fulani linalokusudiwa kwa mtindo wa maandishi ya nathari.

Aina za insha

Insha kwa kawaida huwa ni za aina nyingi kutokana na namna zinavyotungwa. Aina hizo ni hizi zifuatazo:

- Insha za maelezo (Insha za wasifu)
- Insha za masimulizi
- Midahalo na mijadala
- Insha za mazungumzo
- Insha yakinifu

Mambo ya kuzingatia katika utungaji wa insha

- a) Tafuta mawazo yote katika somo hilo na kuandika mawazo muhimu yasipungue manne au matano hii.
- b) Yapange mawazo kufuatana na umuhimu wake katika somo hilo au yapange mawazo kufuatana na mtiririko wa mantiki katika habari hiyo.
- c) Angalia, usiandike nje ya kichwa cha habari. Fuata mpango wa mawazo kama ulivyoyapanga.
- d) Ukishamaliza kuandika utungaji, rudia kusoma habari yote na kufanya masahihisho.



INSHA ZA MAELEZO (INSHA ZA WASIFU)

Katika insha za aina hii, tunatoa wasifu. Tunatoa maelezo kuhusu jinsi kitu, mahali au mtu alivyo au anavyoonekana, yaani sifa zake kitabia, kisura au kimaumbile pamoja na maisha yake. Insha za maelezo pia zinaweza kuwa zinafafanua jinsi kitu au mtu anavyohusiana na mwingine ama tajriba tuliyonayo kuhusu mambo na matukio fulani katika maisha ya siku hadi siku.

Insha za maelezo zinawasiri kwa kutumia maneno ili kufikia lengo na kutoa taathira (dosari, kasoro) ya usanii ya uchoraji au mchongaji wa vjnyago. Kwa maelezo yaliyo katika maandishi, mchoraji anaweza kuchora picha inayofanana na taswira (picha) inayotokana na maelezo hayo. Aya ya insha ya maelezo ni kama picha iliyotokana na kamera.

Madhumuni hasa ya insha ya maelezo ni kutaarifu, kuwaelekeza wasomaji kuhusu mambo ili wayafahamu, kuwaeleza wasomaji ili waelewe kitu au jambo, kuvitambulisha vitu na mara nyingine maelezo yanakusudiwa kuwa burudani.

Inapa swa insha ya wasifu igawanywe katika muundo wenye sehemu tatu kama ilivyo desturi kwa aina zote za insha.

- **Utangulizi**
- **Kiini cha maelezo**
- **Hitimisho**

a) Utangulizi

Insha ya maelezo inaweza kuanza kwa sentensi mada, na kasha maelezo ya kinaganaga kuhusu sentensi mada. Katika sehemu ya utangulizimwanafunzi anaweza vilevile kutoa kisa ijapo kifupi ili kubainisha jambo au kitu anachokusudia kueleza. Hata hivyo, kisa kinaweza kuwa sehemu ya mwili au hitimisho la insha.

b) Kiini cha maelezo

Katika sehemu hii ya insha za wasifu, maelezo yanayotolewa wasifu wa mtu, basi mwandishi anahitajika kutoa maelezo kuhusu:

- Jina lake
- Sifa zake kimaumbile na kisura
- Hulka na desturi zake
- Elimu yake
- Shughuli anazofanya
- Fikra na falsafa zake
- Mapendekezo yake

Iwapo ni wasifu wa mahali, basi mwanafunzi anatakikana kutoa maelezo juu ya:

- Jina la mahali hapo
- Sifa za mandhari ya mahali hapo kama vile majengo yaliyopo viamboni (mahali waishipo watu, kijiji) na maumbile
- Watu wanaostakimu mahali hapo
- Mila, imani, hulka na silica (tabia za kuzaliwa alizo nazo mtu) za watu hao
- Shughuli za wakazi wa mahali hapo

Mambo yafuatayo yanapaswa kutiliwa maanani wakati wa uandishi wa insha za maelezo:

- Inatakikana kutoa maelezo kwa utondoti yaani kinaganaga bila ya kuacha mambo yoyote muhimu.
- Maelezo yawe yanalenga kufunua milango yote ya hisia ya msomaji, hususan kuona, kusikia, kugusa, kuonja na kunusa.
- Uteuzi wa mambo yanayolenga kutoa picha bayana inayokusudiwa akilini mwa msomaji.
- Uteuzi wa msamiati mwafaka wenye kuonyasha ama kutoa picha inayotakikana bila kupoteza maana iliyokusudiwa. Kwa ajili hiyo katika uandishi wa insha za maelezo inampasa mwanafunzi kutumia vivumishi, vielezi na virai

vilivyoteuliwa kwa uangalifu. Aidha matumizi ya misemo, nahau na tamathali za usemi kama vile tashbiha na sitiari huipatia insha uhai na uhalisi wa kupendeza.

- Aidha, maelezo yaandikwe kwa kutilia maanani madhumuni yale na msomaji mlengwa.

Ili kupata picha ya wazi, mwanafunzi anaweza kulinganisha vitu au mambo yanayoelezwa na vitu halisi. Inapasa vitu, watu, mahali au matukio yanayoelezwa yaonekane yana uhalisi machoni mwa msomaji. Hivyo, mwanafunzi aeleze mambo kama yalivyo na sivyo ayadhaniavyo.

Yapasa maelezo yapangwe katika mtiririko mzuri ulio na mantiki. Yawe na mshikamano au mwoano baina ya aya na aya. Mwanafunzi aeleze taratibu kila kipengele cha mada ili kumwzesha msomaji kupata dhana, hisia na picha kamilifu ya kitu ijapokuwa hajapata kukiona, pahali panapoelezwa hajapata kupafika au mtu anayelezwa hajapata kumtia machoni. Kwa hiyo basi, inampasa mwanafunzi awe na ufahamu mzuri wa taswira anayokusudia kutoa ili taathira inayotakikana ionekane waziwazi.

Katika kupaeleza mahali au eneo fulani, mwanafunzi ahakikishe kuwa taathira ya wazi inajitokeza. Anaweza kutofautisha vitu kwa kuvilinganisha.

Kwa mfano:

Majira ya baridina ya kiangazi,

Msimu wa mvua za masika na vuli.

Vile vile, ni muhimu kuhusisha mandhari, mahali na watu walio katika mazingira hayo, ili kuonyesha sifa za watu zinavyohusiana na mazingira yao.

c) Hitimisho

Katika hitimisho la insha ya maelezo inapasa kutoa maelezo ya jumla lakini kwa muhtasari kuhusu mada au jambo. Kisa kinachosadifu jambo lililoshughulikiwa katika insha kinaweza kuwa njia nzuri ya kuugusa moyo wa msomaji. Hitimisho liwe zuri na liwe linakamilisha mawazo na maelezo ya insha nzima.

**MAZOEZI**

1. Yaeleze maonyesho ya kilimo uliyepata kuudhuria. Eleza mambo yaliyokuvutia katika maonyesho hayo.
2. Mweleze rafiki yako unayempenda sana, ukitaja mambo yanayokupendeza katika rafiki yake.
3. Ueleze mtaa, kijiji au mji wenu, ukitaja mambo yanayokupendeza katika mtaa, kijiji au mji huo.
4. Eleza vivutio vya kitalii nchini Rwanda.
5. Toa maelezo kuhusu mchezo wowote wa kuigiza ulioutazama. Eleza mambo yaliyokupendeza au kutokupendeza katika mchezo huo.



SURA YA SITA: AINA ZA MANENO

Wataalamu wengi wa sarufi ya Kiswahili sanifu wanaelekea kukubaliana kwamba katika lugha hii kuna aina za maneno zisizopungua saba. Aina hizi za maneno zimewahi kujadiliwa kwa kina katika vitabu kadhaa vya sarufi vinavyojishughulisha na sarufi miundo na sarufi maumbo.

Aina hizo ni kama nomino/majina, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, vielezi, vihusishi/viunganishi, vihisishi/viingizi.

1. NOMINO/MAJINA

Nomino ni neno linalotaja jina la mahali, mtu, kitu, hali au tendo. Nomino huwa na mgawo wa mafungu saba. Na kila fungu lina majina yenye tabia sawa. Mafungu hayo ya sehemu ni kama ifuatavyo:

a) Majina ya mguso

Haya ni majina ya vitu ambavyo tunaweza kuvigusa, kuvionja na hata kuvishika. Mifano ya majina kama haya ni: kalamu, wanafunzi, ubao, kitanda, pesa, daftari, taa, meza, kisahani, unyasi, n.k.

Majina haya ya mguso yaweza kuwa ya kitu kimoja kimoja, ya wingi, ama hata ya jamii.

b) Majina ya kawaida

haya nayo ni majina ya vitu vyenye maumbile sawa, na viwezavyo kupatikana kwingi. Inapokuwa vitu hivi vya majina ya kawaida ni mambo ya kufikirika tu, majina haya huweza kuingizwa katika kundi la majina ya dhahania, na inapokuwa ni vitu ambavyo hugusika, huingizwa katika kundi la majina ya mguso.

Mifano ya majina ya kawaida ni kama: nyumba, maji, chakula, maua, elimu, upendo, mtu, hewa, mbingu, ubaya, vazi, wema, n.k.



c) Majina ya dhahania

Majina haya nayo ni majina ya vitu ambavyo huweza kufikirika tu na wala havigusiki ama kuonekana. Kwa mfano, vitendo mbalimbali ama matukio fulani fulani, tabia na hali. Mathalan, ni mambo ambayo hatuwezi kuyagusa isipokuwa tunaweza kuyawaza na labda kuaona taswira (picha) yake.

Mifano ya majina ya dhahania ni kama vile: malaika, Mungu, uwezo, njaa, ibilisi, woga, haya, nuksi, uchoyo, ugonjwa, wema, hasara, ukweli, bahati, werevu, n.k.

d) Majina ya pekee

Haya ni majina ya watu ama vitu ambavyo havina maumbile ya namna moja na havipatikani kwa wingi kila pahali. Kwa mfano, mwezi wa Machi wa mwaka wa juzi hauwezi kuwa sawa na mwezi wa Machi wa mwaka huu, hata ingawa yote miwili ni miezi ya Machi.

Nayo mifano zaidi ya majina ya pekee ni kama majina ya watu, miezi ya pekee ni kama majina ya watu, miezi, miaka, pahali, siku za wiki na kadhalika, kama vile: Juma, Januari, Mei, 1995, Mwanza, Kigali, Alhamisi, Jumamosi, 1951, Kaloleni, n.k.

Kutokana na mifano hii yote utaona wazi kuwa majina ya pekee huandikwa kutanguliziwa herufi kubwa kama vile “Mungu”.

e) Majina ya jamii

Watu, vitu ama wanyama wanaweza kuunganishwa wakawa kundi moja kwa sababu ya tabia, hali ama cheo. Wanapounganishwa hivyo, kila kikundi huweza kupewa jina moja linalokitaja kikundi hicho kizima, huku likaleta maana ya kitu kimoja kimoja katika kundi hilo. Basi vikundi kama hivyo ndivyo viwekwavyo katika namna hii ya majina.

Mifano ya majina ya jamii ni kama vile: kundi, shada, koja, tonge, umati, mlolongo, korija (vitu vya aina moja), n.k.



f) Majina ya wingi

Vipo baadhi ya vitu ambavyo daima hupatikana katika hali ya wingi wake tu. Kwa kawaida huwa kazi pevu kujaribu kuvitenganisha vitu hivyo kimoja kimoja na baadhi yavyo havitenganishiki kabisa. Mathalan, ni vigumu kupata mchanga “mmoja” na umande “mmoja”. Unaweza kupata tone la umande, lakini umoja tu haiwezekani.

Mifano zaidi ya majina ya wingi ni kama: maji, maziwa, sukari, nyama, chai, mafuta, uji, bia, unga, rangi, marashi, n.k.

Kutokana na mifano hii, utaona wazi kuwa baadhi ya majina yamo katika umoja (uji), na mengine katika wingi (mafuta), lakini dhana ni ile ile kuwa hayatenganishiki. Ni majina ya vitu kama hivi ambayo huwekwa katika fungu hili la majina ya wingi.

g) Majina ya kitu kimoja kimoja

Haya ni majina ya vitu ambavyo vinaweza kuwekwa pamoja na halafu vikatenganishwa vikawa bado viko kama hapo awali.

Mifano ya majina ya vitu hivyo ni kama yafuatavyo: ndoo, kijiko, kitabu, kalamu, kikombe, chetezo, n.k.

MAZOEZI 1

1. Bainisha maneno yafuatayo yako katika kundi gani la nomino:
 - a) mkulima, uvuvi, ufugaji, usomi
 - b) mtu, mbuzi, ng'ombe, simba
 - c) familia, jamaa
 - d) malaria, UKIMWI, kaswende

2. VIVUMISHI

Kivumishi, kama ilivyo kawaida, ni neno linaloongezea jina maana. Isitoshe, kivumishi ama sifa huweza pia kujiongeza maana. Kwa mfano, unaweza kusema:

Nguo nzuri

Neno “nguo” ni jina na “nzuri” ni kivumishi kinachoongeza “nguo” maana.

Ama ukisema: **Nimenunuliwa nguo nzuri nzuri;**

Neno “nzuri” la mwisho ni kivumishi kinachoongeza maana kivumishi kingine, yaani “nzuri” ya kwanza.

Vivumishi vinaweza kugawika katika migawo miwili tofauti.

Kwanza, upo mgawo ambapo kuna vivumishi vichukuavyo viambishi na vipo vile ambavyo havichukui viambishi. Mathalan, kivumishi “-zuri” huchukua kiambishi. Lakini kivumishi “tajiri” ama “ghali” hakichukui kiambishi.

Pili, vivumishi vinaweza kugawika katika makundi ama mafungu kadhaa kulingana na matumizi yake. Mafungu hayo ya mgawo huu kwa muhtasari ni haya:

- i) Vivumishi vya idadi: ni vivumishi vinavyoonyesha jumla au hesabu ya vitu. Aina hii ya vivumishi tunaweza kuigawa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lile linaloonyesha idadi kwa ujumla na kundi la pili ni lile linaloonyesha idadi kwa hesabu. Vivumishi vinavyoonyesha idadi ni kama hivi vifuatavyo: chache, ingi, haba, pungufu, maridhawa, kidogo, moja, mbili, tano, ishirini, mia, elfu, milioni, n.k.
- ii) Vivumishi vya sifa: ni vivumishi vinavyotaja tabia au namna vitu vilivyo au vinavyoonekana. Vivumishi vinavyoonyesha tabia hii ni kama hivi vifuatavyo: ema, pevu, nyamavu, nyenyekevu, danganyifu, changamfu, zuri, baya, bovu, refu, kubwa, pya, eusi, pana, kamili, rahisi, safi, n.k.
- iii) Vivumishi vya pekee (-enye, -enyewe, -ingine, -ote)
- iv) Vivumishi vya **-A** unganifu (wa, cha, vya, ya, la, za, pa, mwa, na kwa)
- v) Vivumishi vya jina kwa jina
- vi) Vivumishi vya **Ki-** ya mfanano
- vii) Vivumishi vya jina kwa kitenzi

viii) Vivumishi viulizi: ni vivumishi vinavyouliza maswali kuhusiana na nomino inayoandamana navyo. Kama vile: watu wangapi?, miti mingapi?, mayai mangapi?, n.k.

ix) Vivumishi vimilikishi

x) Vivumishi vionyeshi/viashiria

Ukivichukua vivumishi hivi kimoja kimoja, utapata kuwa matumizi ya kila kivumishi ni tofauti.

MAZOEZI 2

1. Je, vivumishi ni nini?
2. Je, vivumishi vinaweza kugawanyika katika makundi mangapi kimaumbo? Yataje.
3. Jadili aina zifuatazo za vivumishi.
 - a) vivumishi vya idadi
 - b) vivumishi vya pekee

3. VIWAKILISHI

Viwakilishi huitwa pia vijina au vibadala. Navyo ni maneno ambayo husimama badala ya majina ili kujulisha kitu kinachohusika. Maneno haya yanapotumika, jina la kitu kinachosimamiwa halitajwi.

Kundi hili la maneno linaweza kugawika katika sehemu tano. Sehemu hizi ni kama ifuatavyo:

- i) Viwakilishi nafsi (mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi, wao)
- ii) Viwakilishi viulizi (yupi, zipi, yapi, wepi, upi, kupi, ipi, lipi, papi, n.k.)
- iii) Viwakilishi vibainishi (ambaye, ambacho, ambao, ambamo, ambako, ambalo, n.k.)
- iv) Viwakilishi vimilikishi (wangu, kwake, letu, vyao, pao, wenu, n.k.)
- v) Viwakilishi onyeshi (huyu, hawa, huyo, hao, Yule, wale, hilo, huo, lile, n.k.)

MAZOEZI 3

1. Eleza kwa ufupi dhana ya viwakilishi.
2. Tunga sentensi tano zinazoonyesha viwakilishi viulizi.
3. Kuna viwakilishi nafsi vingapi katika lugha ya Kiswahili?
4. Bainisha viwakilishi vilivyomo katika tungo zifuatazo:
 - a) Lile linakwenda wapi?
 - b) Wangu mimi ananiumiza roho.
 - c) Wale mliowaona walipigwa sana.
 - d) Ambao wamechelewa wataadhibiwa vikali.

4. VITENZI

Kitenzi ni neno likuarifulo jambo la kufanya au linalofanywa. Tofauti iliyopo kati ya kitenzi na kitendo ni kwamba kitenzi ni neno likujulishalo kitu cha kufanya kama vile “soma” na ni neno tu. Unapoanza kukitimiza unachoambiwa ufanye, yaani kusoma, kitendo kinatokea. Kwa hivyo, kitenzi ni neno lakini matokeo yake ni kitendo.

Mifano ya vitenzi ni kama: pika, imba, guguna, beba, soma, samehe, rudi, tubu, dhani, dhuru, n.k.

Hata hivyo, vitenzi vinaweza kugawika katika migawo mingi kutegemea lengo la anayegawa. Mojawapo wa migawo hiyo ni vitenzi vyenye asili ya Kibantu na vile vyenye asili ya kigeni. Vitenzi vya asili ya Kibantu huishia kwa **-a**, kwa mfano:

Paka, kata, nona, sema, lewa, ruka, ziba, koma, zuka, tema, juta, kwea, peta, n.k.

Kuna pia baadhi ya vitenzi vya kigeni viishiavyo kwa **-a**. Vitenzi kama hivyo ni: rejea, duwaa, amia, shiba, hitilafiana, nuia, hatarisha.

Mbali na vitenzi hivi vya kigeni viishiavyo kwa **-a**, vipo vingine ambavyo huishia kwa **-e**. nayo mifano ya vitenzi hivyo ni:

starehe, samehe, baleghe.

Hali kadhalika, vitenzi vivyo hivyo vya kigeni huwa na kundi liishialo kwa **-i**.

Kwa mfano: rudi, ishi, dhani, kubali, dai, kiri, safari, saliti, kejeli, ajiri, n.k.

Mwisho, vipo vitenzi vya kigeni ambavyo hishia kwa **-u**. Nayo mifano hapa ni kama vile: ruhusu, fahamu, shutumu, thubutu, jibu, sahau, shukuru, tubu, dhulumu, sifu, lazimu, n.k.

kut okana na mifano hii yote, utaona kuwa hapana vitenzi viishiavyo na **-o** na pia kwamba vitenzi karibu vyote viishiavyo na **-e**, **-i** ama **-u** huwa vya asili ya kigeni. Hata hivyo, muundo wa matumizi ya vitenzi ni huo huo tu, view ni vya asili ya kibantu ama la.

5. VIELEZI

Kielezi ni neno linaloongezea kitenzi maana. Pia huweza kuongezea sifa maana na pia kujiongezea maana. Matumizi haya matatu yote ni muhimu katika sarufi ya Kiswahili.

Ukianza na matumizi ya kwanza, unapata kuwa kitenzi huongezewa maana na kielezi ambacho pia huitwa kisifa. Kwa mfano, unaweza kusema:

Mkufunzi alitembea haraka.

Neno “haraka” linakujulisha jinsi kitendo cha kutembea kilivyofanywa.

Pili, kielezi hujiongezea maana hivi:

Mwanafunzi alitembea haraka mno.

Hapa, kielezi “mno” kimeongezea maana kielezi kingine “haraka”. Tatu, kielezi huweza kuongezea kivumishi maana hivi:

Mkufunzi mwerevu sana yuaja.

Hata hivyo, vielezi vinaweza kugawika katika mafungu tofauti kulingana na matumizi yavyo katika sentensi. Nayo mafungu hayo ni haya:

- i) Vielezi vya wakati (asubuhi, zamani, Januari, mtondo, jioni, Alhamisi, lini, 1944, kesho, juzi, wakati wa njaa, n.k.)

- ii) Vielezi vya mahali (kwetu nyumbani, ndani ya, kule Mombasa, n.k.)
- iii) Vielezi vya kiasi au idadi (mara moja, mara mbili, mara elfu, mara saba, n.k.)
- iv) Vielezi vya namna (kinagaubaga, bure, hima, sawa, hasa, ovyo, barabara, rejareja, n.k.)

MAZOEZI 4

1. Nini maana ya vielezi.
2. Bainisha vielezi vilivyoandikwa kwa hati nzito ya mlalo katika sentensi zifuatazo:
 - a) Anakunywa **haraka haraka**
 - b) Hamisi amecheza **vibaya** mchezo huu
 - c) Usimwamshe, amechoka **sana**
3. Taja aina mbili za vielezi.

6. VIUNGANISHI/VIHUSISHI

Vihusishi, viunganishi ama vihusiano ni maneno ambayo huunganisha maneno mengine mawili ama zaidi. Maneno haya hasa huonyesha uhusiano baina ya neno na neno au fungu hili la maneno ya fungu jingine. Katika huku kulinganisha sehemu mbalimbali, vihusishi huweza kutudokezea uwiano wa kisarufi unaotonyesha jinsi uhusiano wa vitu vilivyotajwa ulivyo au jinsi mambo fulani yanavyosimama katika ujirani ama ushirikiano miongoni mwao.

Hata hivyo, vihusishi navyo huweza kujigawa katika mafungu mawili. Vipo vihusishi vyenye asili ya **-a** unganifu na vipo vihusishi mkopo. Ukichunguza vihusishi vya **-a** unganifu unapata kuwa maneno haya huundwa kwa kuunganisha viambishi ngeli na **-a** unganifu. Hili linapotendeka, hupatikana maneno haya: wa, vya, pa, na, cha, la, mwa, ya, za, kwa.

Baadhi ya maneno haya yanapotumiwa pamoja na majina ya dhahania, wakati au hata mahali, mafungu ya vivumishi hutokea. Kwa mfano, unapata: mbele ya, nyuma ya, mahali pa, ukingoni mwa, nje ya, upande wa, miongoni mwa kadiri ya, n.k.

Pili vipo vihusishi mkopo. Katika fungu hili, hupatikana maneno ambayo yakiangaliwa kimuundo inapatikana kuwa hayatokani na **-a** unganifu. Maneno hayo hasa huwa na asili ya kigeni kama vile Kiarabu ama hutokana na maneno mengine ya Kiswahili ambayo hayahusiani na **-a** unganifu. Majina, vielezi na vitenzi huweza kuwa ni asili ya vihusishi hivi mkopo. Hasa baadhi ya majina, vitenzi na vielezi huwza kutumika kama vihusishi kwa kuangaliwa upatanisho wayo kisarufi.

Mifano ya vihusishi mkopo ni: kupita, basi, yaani, lakini, hadi, mpaka, tangu, ila, kulingana na, bila, bali, kuliko, katika, labda, tena, hata, pasipo.

MAZOEZI 5

1. Viunganishi ni nini?
2. Tunga sentensi nne ambazo huonyesha viunganishi.
3. Tunga sentensi ukitumia viunganishi vifuatavyo:

a) japo	d) wala
b) au	e) katika
c) kwa	f) kama

7. VIINGIZI/VIHISISHI

Kiingizi ni neno linaloonyesha hangaiko la moyo ama kudokeza mguso wa moyo ama hata wa akili. Nayo mahangaiko ama miguso ya moyo huwa tofauti tofauti. Kwa mfano, kuna kukosekana kwa matumaini, furaha na laana pia. Isitoshe, kuna huruma, mshangao, hasira, wasiwasi na kadhalika. Ili kuonyesha baadhi ya mahangaiko haya, yapo maneno fulani fulani yanapotumiwa. Maneno hayo, kinyume na mengine mengi yaliyotajwa hapo awali, si ya lazima katika sentensi. Hata hivyo, yanapotumiwa huweza kuongeza ufasaha mwingi katika usemi.

Mifano ya baadhi ya viingizi ni hii ifuatayo: ati/eti, ala!, alaa!, basi, afanaalek, ajabu, pole, sasa/tena, haki ya Mungu, ewe, inshallah, ohoo, kumbe, oyee, zii, wallah.

Mifano katika sentensi:

- Haki ya Mungu, mimi sikuiba.
- Rais Kagame, oyee!
- Ala! Vipi mtu kujitia wazimu namna hii!
- Afanaaleh! Nimesahau kabisa kuwa leo ni siku ya kuzaliwa kwangu.

MAREJEO

- Chiraghdin, S. na Mnyampala, E.M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi. OUP.
- Cooperative TRAFIPRO (1982). *Tujifunze Kiswahili*. Kigali.
- Direction des Programmes de l'Enseignement Secondaire (1986). *Kitabu cha Kiswahili IV-V A*.
- Kihore, Y.M, Massamba, D.P.B., Msanjila, Y.P. (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.
- Massamba, D.P.B. (2002). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi. OUP.
- Mazrui, A.M. na Syambo, B.K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. East African Educational Publishers Ltd. Nairobi.
- Mbunda Msokile (1993). *Msingi ya uhakiki wa Fasihi*. East African Educational Publishers Ltd. Nairobi.
- Mohamed, A.M. (1986). *Sarufi Mpya*. Press and Publicity Centre. Dar es Salaam.
- NDALU, A. (1997). *Mwangaza wa Kiswahili*. East African Educational Publishers. Nairobi-Kampala.
- Nkwera, F.M. (1978). *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyu*. DRM, TPH.
- Polycarp S. Wekesa (2000). *Uandishi wa Insha*. Acacia Stantex Publishers Muthithi House, Westlands. Nairobi.
- Rocha, C. (2005). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi.
- Rwabushaija, M. (1999). *Masomo ya Msingi wa Kiswahili*. Fountain Publishers Ltd, Kampala.

- Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987). *Kitabu cha Kiswahili IV B*. Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari. Kigali.
- Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987). *Kitabu cha Kiswahili IV-VA*. Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari. Kigali.
- TUKI (2002). *Fasihi Simulizi: Vitendawili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA NNE MKONDO WA LUGHA ni kitabu ambacho kimetayarishwa baada ya kuona tatizo la kutokuwepo vitabu vya Kiswahili vya kutosha katika shule za upili kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma lugha hii. Kitabu hiki kimeandikwa na walimu wanaojifunza Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kigali (KIE). Masomo yaliyomo katika kitabu hiki, yanafuata muhtasari wa mafunzo ya somo la Kiswahili. Masomo haya ambayo anakiunda kitabu hiki yatawezesha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kuwa rahisi na kueleweka vizuri kwa kila mwanafunzi anayesoma lugha ya Kiswahili.